# Nipashe

Ijumaa Aprili 19, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579896

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Msichana anayesumbuliwa ugonjwa wa ajabu asimulia

UKURASA 3




UKURASA 13

# Ofisi za mabati zageuka kivutio

• **Wananchi** wamiminika kupata huduma... *Ukurasa 2*





Baadhi ya watumishi wa serikali wakisubiri huduma nje ya Ofisi ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), eneo la Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma jana. **Picha ndogo:** Naibu Katibu Mkuu Tamisemi, Dk. Dorothy Gwajima, akiendelea na kazi ofisini kwake. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Ngome ya Mbowe Hai yavunjwa

UKURASA 26






## Wabunge walia kuminywa uhuru vyombo vya habari

UKURASA 2

HABARI KITAIFA

## Sugu asusa kusoma hotuba yake bungeni

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI Kivuli katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Joseph Mbilinyi, maarufu Sugu, jana alisusa bungeni kusoma hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kutokana na uongozi wa Bunge kuagiza kufutwa kwa baadhi ya maneno yaliyoko kwenye kitabu cha hotuba hiyo.

Mara tu baada ya Sugu kuanza kusoma hotuba yake hiyo, Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alimkatisha waziri kivuli huyo kusoma taarifa ambayo wanayo wabunge wengine, ambayo baadhi ya maneno yalikuwa yamefutwa.

Hata hivyo, Sugu alisema hawezi kusoma hotuba yake kwa kuwa anachotakiwa na uongozi wa Bunge kukisoma ndani ya Bunge siyo maoni yake bali maneno ya kulishwa.

Sugu alisema imekuwa kawaida ya Kiti cha Spika kuizuia hotuba yake kusomwa bungeni, akieleza kuwa hizo ni dalili za uoga wa serikali.

Kutokana na uamuzi huo wa Sugu kutosoma hotuba yake bungeni, Naibu Spika (Dk. Ackson) aliagiza hotuba hiyo isiwekwe katika kumbukumbu za taarifa za Bunge.

Baadaye, akichangia mjadala wa hoja ya makadirio ya bajeti ya wizara hiyo, Sugu alisema pamoja na kuwapo kwa idadi kubwa ya vyombo vya habari nchini, bado hakuna uhuru wa habari.

Sugu alisema Bunge pia limebariki hali hiyo kwa kuruhusu mijadala yake kutoonyeshwa moja kwa moja (live).

**BAJETI UWANJA WA TAIFA**

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Peter Serukamba, alisema kamati yake imebaini bajeti ya kutekeleza miradi ya maendeleo ya wizara imepungua.

"Si hivyo tu, lakini pia mradi wa ujenzi eneo la Changamani la Michezo na husiusan Uwanja wa Taifa na Uhuru haujatengewa fedha wakati mkataba baina ya nchi yetu na Jamhuri ya Watu wa China unafikia ukingoni mwezi Agosti 2019.

"Ikumbukwe kuwa wastani wa gharama za uendeshaji wa Uwanja wa Taifa na Uhuru ni takribani Sh. milioni 781 kwa mwaka," Serukamba alibainisha.

Alisema kamati yake inaishauri serikali kwa mara nyingine kuongeza bajeti ya maendeleo kwa wizara hiyo ili zipatikane fedha kwa ajili ya uendeshaji na ukarabati wa Uwanja wa Taifa na Uhuru.

Aliongeza kuwa kamati inaipongeza serikali kwa kuanzisha chaneli ya utalii (Tanzania Safari) kwa lengo la kuvutia watalii.

# Ofisi za mabati zageuka kivutio

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

UTEKELEZAJI wa agizo la Rais la wizara zote 23 kuhamia katika Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma limetekelezwa, huku Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), ikiwa kivutio kwa wananchi.

Ofisi hiyo imekuwa kivutio kikubwa kwa watu wanaotembelea mji huo kutokana na kuwahudumia wananchi, huku wakiwa katika ofisi za mabati.

Nipashe jana, ilitembelea wizara hizo katika mji huo na kushuhudia wananchi wakiingia na kutoka kupata huduma.

Jengo la ghorofa mbili la ofisi hiyo halijakamilika na kusababisha viongozi wake kuendelea kuwahudumia wananchi ndani ya mabanda ya mabati yaliyopo kwenye jengo hilo yaliyokuwa yanatumiwa na mkandarasi.

Mwandishi wa gazeti hili alishuhudia Waziri na Katibu Mkuu wanatumia ofisi moja, manaibu waziri pia wanatumia ofisi moja na kwa upande wa manaibu makatibu wakuu nao wapo katika ofisi moja tofauti na awali kila kiongozi alikuwa na ofisi yake.

Pia Idara ya Utawala ya Ofisi hiyo inatumia ofisi yake ya kujitegemea.

Nipashe ilikutana na Naibu Katibu Mkuu Tamisemi anayeshughulikia afya, Dk. Dorothy Gwajima, ambaye alikuwa akitekeleza majukumu yake.

Akizungumzia utekelezaji wa agizo la Rais, Dk. Gwajima, alisema watu wamekuwa wakifika katika ofisi hizo kujiridhisha kama kweli viongozi hao wanatumia ofisi za aina hiyo.

"Ni kweli tunatumia hizi ofisi wala wasifikirie wanaigiza," alisema.

Aidha, aliwataka wafanyakazi wa wizara mbalimbali kuunga mkono kuweka historia ya kuhamia kwenye mji huo.


Alisema serikali ya awamu ya tano inafanyakazi kwa vitendo, hivyo baada ya agizo la Rais wao wakiwa ni wasaidizi wake wamefanya kwa vitendo kuhamia katika mji huo wa serikali.

"Katika ufanyaji kazi kwa vitendo utakutana na changamoto ngumu hazituridishi nyuma bali tunaendelea kusonga mbele na kuchapa kazi kama kawaida, si unatuona humu tunaendelea kwa kutoa huduma," alisema.

Alitoa mfano kuwa Rais John Magufuli alipokuwa Waziri wa Ujenzi alijenga barabara maeneo mengi nchini na zingine zilionekana kuwa zipo porini, lakini watu wanashangaa maendeleo yalivyofika huko.

Alisema mazingira ya kazi yanatakiwa yaanzie kwenye mioyo ya

INAENDELEA UK. 8



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, akisaidia shughuli za ujenzi wa mradi wa nyumba za askari Magereza Ukonga, akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo mkoani humo jana. Katikati ni Mkuu wa Mradi huo, Brigedia Jenerali Charles Mbuge na (kushoto) ni Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Magereza, Julius Ntambala. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Wabunge walia kuminywa uhuru vyombo vya habari

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BAADHI ya wabunge wamelalamika bungeni kuhusu kile walichoeleza kuminywa kwa uhuru wa vyombo vya habari kunakofanywa na serikali.

Watunga sheria hao walitoa kilio hicho bungeni jijini Dodoma jana, walipochangia hoja ya mjadala wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka ujao wa fedha.

KHATIBU SAID HAJI

Katika mjadala huo, Mbunge wa Konde, Khatibu Said Haji (CUF), alisema licha ya baadhi ya mawaziri kujinadi kuwa kuna uhuru wa vyombo vya habari na kuna vyombo vingi vya habari vilivyosajiliwa nchini, bado hakuna uhuru wa vyombo hivyo katika kutekeleza majukumu yake.

"Jana (juzi) nilimsikia Waziri wa Mambo ya Nje, Prof. (Palamagamba) Kabudi, akisifia nchi yetu juu ya mafanikio makubwa na sifa waliyopata duniani juu ya uhuru wa vyombo habari.

"Alikuwa akizungumza hapa (bungeni) akisema kuwa nchi yetu imepokea sifa kubwa sana juu ya uhuru wa vyombo vya habari. Na moja ya mambo ambayo imesifiwa ni pamoja na kuwa na idadi kubwa ya magazeti, kwa hiyo ilikuwa sifa kubwa kwa nchi yetu. Mimi nadhani alikuwa akielezea aliyokutana nayo huko nje.

"Lakini Mheshimiwa Naibu Spika, siku mbili baadaye nimemsikia Msemaji Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo akiyataka magazeti yaliyoripoti taarifa za uchambuzi wa taarifa aliyoitoa Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto kabwe, chama jirani, yajieleze kwa kuandika uchambuzi wa chama hicho kuhusu ripoti ya CAG.

"Hili jambo kweli limetupa mashaka, anakwenda duniani anapata sifa ya uhuru wa vyombo vya habari, lakini nyuma yake serikali vyombo vya habari kuripoti taarifa ambayo ilitolewa, siyo taarifa ya msituni, ni taarifa iliyokuwa ya wazi na vyombo vya habari wana haki na ni pamona na kutimiza majukumu yao ya kuwaelimisha Watanzania, ni nini kimezungumzwa na kiongozi yule wa chama

INAENDELEA UK. 8



Daktari Bingwa na Mkuu wa Idara ya Upasuaji katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Ibrahim Mkoma (kulia), akimfariji mkazi wa Singida Mariam Rajab Juma (25), aliyelazwa katika jengo la Kibasila Wadi namba 15, hospitalini hapo, jijini Dar es Salaam jana, akifanyiwa uchunguzi wa kidonda sugu kilichopo mgongoni kwake katika bega la kulia. Kushoto ni Ofisa Muuguzi wa Wadi hiyo, Yusta Nchemwa. **PICHA: JOHN BADI**

# Msichana anayesumbuliwa ugonjwa wa ajabu asimulia

**Na Romana Mallya**

MKAZI wa Kitongoji cha Inung'una mkoani Singida, Mariam Rajab (25), mwenye kidonda mgongoni ambaye alionekana mtandaoni akiomba msaada wa matibabu na kupokelewa hospitali ya Muhimbili, amesimulia mateso makali aliyoyapata kwa miaka mitano.

Mariam ambaye alipokelewa usiku wa kuamkia jana Hospitali ya Muhimbili na sasa amelazwa wodi namba 15 jengo la Kibasila, amesimulia alivyoteseka na kidonda hicho ambacho chanzo chake ni moto.

Msichana huyo alisimulia kuwa miaka mitano iliyopita baada ya kuungua na moto eneo hilo la mgongo, alitibiwa hospitali ya Mkoa wa Singida hadi kilipoonekana kimepona.

Alisema baada ya kupona kovu la moto eneo hilo la mgongo lilitokea jipu ambalo baadaye lilipasuka.

"Lilipopasuka nikawa nakwenda hospitalini kusafishwa, lakini kadri siku zilivyoendelea kidonda kiliongezeka na gharama za kusafishwa kila siku ilikuwa ni Sh. 5,000, kama nilivyoeleza familia yetu ni maskini hivyo haikuweza kuzimudu," alisema.

Mariam alisema aliendelea na huduma ya kusafishwa kila siku hospitali na kuanzia Agosti mwaka jana ilibidi awe anapewa huduma hiyo nyumbani na ndugu zake kutokana na hali ya kimaisha waliyonayo.

"Kadri kilivyokuwa kinasafishwa nyumbani kidonda kikawa kinaendelea kukua na mwisho wa siku kikafikia ukubwa huu, wakati nasafishwa nyumbani kuna mtu alituambia kuwa naweza kutumia unga wa

INAENDELEA UK. 8

# Serikali yatangaza kampeni kurudisha fuvu la shujaa

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imetangaza kampeni ya kurudisha fuvu la shujaa mwanamke, Leti Hema, kutoka Kabila la Wanyaturu ambaye kichwa chake kilikatwa na Wajerumani kisha kupelekwa Ujerumani wakati wa mapambano dhidi ya ukoloni.

Kampeni hiyo ilitangazwa bungeni jijini Dodoma jana na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alipowasilisha hotuba kuhusu makadirio ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

"Alipouawa shujaa huyo, wakoloni hawakuridhika waliamua kukata kichwa chake na kukipeleka Ujerumani kwa uchunguzi wa kina kubaini kama alikuwa na uwezo maalum wa kibaiolojia wa kufundisha wadudu wadogo wenye ubongo mdogo kama nyuki," Dk. Mwakyembe alisema.

Waziri huyo aliendelea kueleza kuwa shujaa huyo alisimama kidete kuzuia utawala wa Kijerumani kwa zaidi ya miaka mitatu akitumia makundi ya nyuki waliowang'ata wazungu pekee.

Alisema nyuki hao waliwazuia Wajerumani kufika kwenye Kilima cha Ng'ongo Ipembe na maeneo yanayozunguka eneo la sasa la Singida Mjini.

"Mbali na hayo, shujaa huyo alionyesha miujiza alipokutana na Wajerumani kwa mazungumzo yaliyovunjika kwa kukaa juu ya ncha kali ya mkuki badala ya kigoda cha kawaida," Dk. Mwakyembe alisema.

Waziri huyo alisema shujaa huyo na wengine walioshiriki harakati za ukombozi wakiwamo Mtemi Isike wa Tabora aliyepigana na Wajerumani kwa zaidi ya miaka minne na Nduna Mkomanile wa Wangoni, hawajaandikwa wala mchango wao kuthaminiwa katika historia.

Alibainisha kuwa mbali na kufufua kampeni ya kurejesha nchini fuvu hilo, wizara yake itasimamia kampeni ya kuhimiza watafiti kuandika upya historia ya ukombozi wa taifa.

Dk. Mwakyembe alisema serikali inaendelea kuandaa sheria itakayosimamia uhifadhi na uendelezaji wa maeneo yenye historia ya ukombozi wa nchi na Afrika.

"Vilevile, uliandaliwa mpango wa kikanda wa miaka mitano wa utekelezaji wa programu ya pamoja na mpango wa kitaifa wa miaka mitano ambao umewasilishwa kwa wadau wa ndani na nje ya nchi kwa utekelezaji wa vipaumbele na malengo ya mipango hiyo," alisema.

Dk. Mwakyembe aliongeza kuwa kwa mwaka wa fedha 2019/20, Baraza la Kiswahili (Bakita) litaandaa vipindi 600 vya redio na televisheni vya kuelimisha umma kuhusu matumizi fasaha na sanifu ya Kiswahili.

Pia kutakuwa na usanifishaji istilahi 300 za nyanja mbalimbali, kutambua na kusajili taasisi na vituo 20 vinavyofundisha Kiswahili kwa wageni na kuongeza matini za maneno 500,000 ya kongoo la Kiswahili.

Alitaja majukumu mengine ni kuendelea kusajili wataalamu wa Kiswahili katika kanzidata iliyoanzishwa, kuendesha semina 10 kwa waandishi na watangazaji wa redio na televisheni.

Ili kutekeleza majukumu ya wizara katika mwaka ujao wa fedha, Dk. Mwakyembe aliliomba Bunge kuidhinisha bajeti ya Sh. bilioni 30.879. Kati yake, Sh. bilioni 15.483 ni mishahara, Sh. bilioni 9.396 ni matumizi mengineyo na Sh. bilioni sita za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

# Maeneo ya ujenzi wa viwanda vya mifuko ya karatasi yatengwa

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki, amesema wanatarajia kufanya mazungumzo na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), ili kutenga maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya kuzalisha mifuko ya karatasi nchini.

Kairuki alisema hayo jijini Dar es Salaam jana, katika mkutano wa uwekezaji ulioandaliwa kwa ushirikiano wa serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na Ubalozi wa China nchini.

Kairuki alitoa wito kwa Watanzania kuchangamkia fursa ya kuwekeza katika uzalishaji wa mifuko ya karatasi kwa kuanzisha viwanda vya kuitengeneza kupitia mtu mmoja au kwa vikundi.

Kairuki alisema ili kulinda soko la ndani watahakikisha wanaweka makatazo mengi katika uingizaji wa mifuko aina ya karatasi kutoka nje ili kuwapa fursa wazalishaji wa ndani.

"Hii ni fursa kubwa ambayo imejitokeza kwa Watanzania kupitia katazo la serikali la kuzuia matumizi ya mifuko ya kubebea mizigo ya plastiki na tutahakikisha tunaweka makatazo mengi hata ikibidi katika aina ya mifuko kama ya karatasi kutoka nje ili kulinda soko la uzalishaji la ndani," alisema Kairuki na kuongeza:

"Ombi langu lingine ambalo pia tutazungumza na Tamisemi waone kwamba ni fursa watenge maeneo kwa ajili ya viwanda vya mifuko ya karatasi kuhakikisha kwamba itakapofika Juni Mosi, mwaka huu, maeneo ya uwekezaji yawe yako tayari, lakini pia na taasisi za kifedha ziwe tayari kuwasaidia wawekezaji wa kitanzania ili wawekeze katika furza hiyo muhimu ambayo imejitokeza."

Alisema inakadiriwa Watanzania wanatumia si chini ya mifuko ya plastiki bilioni tatu kwa kima cha chini na inakadiriwa Mtanzania mmoja kwa wiki anatumia mfuko mmoja mpaka miwili ya plastiki.

"Kwa hiyo kwa fursa hii ambayo imekuja ni kubwa inabidi Watanzania waichangamkie, na tumeambiwa kwamba zipo mashine za kutengeneza mifuko ya karatasi za mpaka Sh. milioni 2,000,000 hadi Sh. milioni 5,000,000, kwa hiyo watu wanaweza kuungana hata kupitia vikundi wakachangamkia fursa hii," alisema Kairuki.

Pia Kairuki alisema ofisi yake itaendelea kuondoa vikwazo vilivyopo katika sekta ya biashara na uwekezaji nchini.

# Jaji Mutungi ataka subira hatima ACT

Na Enock Charles

MSAJILI wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, ametaka pawapo na subira kuhusu hatima ya chama cha ACT-Wazalendo kufutiwa usajili ama la na kuwa ofisi hiyo itatoa taarifa itakapokuwa tayari.

Akijibu swali la mwandishi wa gazeti hili aliyetaka kufahamu hatima ya chama hicho, Jaji huyo alisema ofisi hiyo haifanyi kazi kwa kushinikizwa, na kwamba itatoa majibu pale itakapokuwa tayari kufanya hivyo.

"Unauliza sasa ili iweje... tutatoa taarifa itakapo kuwa tayari," alisema Jaji Mutungi alipoulizwa jana.

Machi 25 ofisi hiyo ilieleza nia yake ya kutaka kukifutia usajili chama hicho na kukipa siku 14 kuanzia Machi 26, kuwasilisha maelezo ya kwanini kisifutiwe unachama wa kudumu.

Hatua hiyo ilichukuliwa ikiwa imepita wiki moja tangu aliyekuwa Katibu Mkuu wa CUF, Maalim Seif Sharif Hamad, kujiunga na ACT-Wazalendo pamoja na waliokuwa viongozi waandamizi wa chama hicho na wanachama wa kawaida.

Msajili aliiandikia barua ACT-Wazalendo yenye kumbukumbu namba HA.322/362/20/98 ya Machi 25, mwaka huu, kujieleza kwanini isifutiwe usajili wa kudumu kwa vitendo vya uvunjifu wa sheria ikiwamo kutowasilisha hesabu za ukaguzi mwaka 2013/14.

Chama hicho pia kinadaiwa kuchoma moto bendera za CUF baada ya mahakama kutoa hukumu iliyompa uhalali Prof. Ibrahimu Lipumba kuwa mwenyekiti halali wa CUF.

Barua hiyo pia imekituhumu chama hicho kutumia dini katika siasa zake baada ya mashabiki kuonekana katika mitandao wakipandisha bendera yao kwa kutumia tamko takatifu la dini ya kiislam (Takbiir), kitendo ambacho Ofisi ya Msajili inasema imekiuka kifungu cha 9(1)c ya Sheria ya Vyama vya Siasa.

Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Zitto Kabwe, ambaye pia ni Mbunge wa Kigoma Mjini, alinukuliwa na vyombo vya habari akidai chama hicho kimewasilisha barua ya maelezo yenye majibu ya hoja walizoulizwa na Msajili.



Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani wakipima ajali ya gari kwenye mzunguko wa Ubungo, unaokutanisha Barabara za Morogoro, Mandela na Sam Nujoma, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Makonda awaombea JWTZ majengo ya NSSF kwa JPM

Na Mary Geofrey

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amemshauri Rais John Magufuli, kuwapa kazi Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) ya kumalizia ujenzi wa majengo ya Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) yaliyoko Tuangoma, Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam.

Makonda alitoa ushauri huo jana wakati akikagua ujenzi wa nyumba za maofisa wa Gereza la Ukonga katika mwendelezo wa ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo katika mkoa huo.

Alisema alitembelea nyumba hizo na kubaini kuwa zimeshaanza kuchakaa ilhali bado hazijakamilika hivyo alimshauri Rais Magufuli kuikabidhi kazi hiyo JWTZ.

"Namuomba Rais John Magufuli akabidhi ujenzi wa nyumba hizi za NSSF kwa JWTZ ili aone kama kuna kitu anaweza kufanya kwa haraka ili yapangishwe kwa wananchi na serikali ipate fedha kuliko kuendelea kuchakaa," alisema Makonda.

Makonda alisema ujenzi wa nyumba hizo ulianza tangu mwaka 2014, lakini hadi sasa haujakamilika licha ya kuwa huduma muhimu zimeshafika katika mtaa huo.

"Katika mtaa ule kuna barabara ya kiwango cha lami kabisa na huduma muhimu zinapatikana kwa hiyo kama majengo haya yatamaliziwa haraka yataanza kutumika na kuiingizia serikali mapato," alisema Makonda.

Kuhusu ujenzi wa majengo ya nyumba za maofisa wa Magereza, Makonda alisema ameridhishwa na ujenzi unaoendelea ambao katika hatua ya msingi umefika asilimia 90.

Alisema ujenzi wa majengo hayo 12 ukikamilika utasaidia familia 172 kupata makazi ya kuishi.

## Daktari aonya uchanganyaji wa dawa za hospitali, kienyeji

Na Happy Severine, BARIADI

DAKTARI bingwa wa magonjwa ya ndani na maradhi ya moyo kutoka Wizara ya Afya, Prof. Harun Nyagori, amewatahadharisha Watanzania kutochanganya dawa za hospitali na kienyeji wakati wa matibabu yao ili kuepuka athari za kiafya.

Prof. Nyagori aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano wa chama cha wanataaluma na wajasiriamali wa Kanisa la Waadventista Wasabato, unaofanyika mjini hapa.

Alisema kuwa uchanganyaji wa dawa za hospitali na za kienyeji ni hatari kwa afya ya binadamu kwa kuwa husababisha kuunda sumu kwa kiasi kikubwa ndani ya mwili wa binadamu.

Aidha, alisema kuwa ni vema wagonjwa mbalimbali wa magonjwa ya ndani na maradhi ya moyo kuamua kufanya maamuzi ya matumizi ya dawa upande mmoja ili wasije kujisababishia madhara makubwa zaidi.

"Napenda kuwashauri wagonjwa wote ambao wako kwenye matibabu, wachague dawa zipi wanaweza kuzitumia, wasichanganye dawa za hospitali na kienyeji...ni vema wakatumia za upande mmoja ili kuepuka athari za uundwaji wa sumu kubwa mwilini...," Nyagori alisema.

Prof. Magori pia aliwahimiza wananchi wa wakazi wa Simiyu kujitokeza kwa wingi kupima afya zao.

Aliongeza kuwa ndani ya siku mbili ambazo wamekuwa wakitoa huduma hizo za magonjwa ya ndani na maradhi ya moyo, jumla ya wagonjwa 269 walijitokeza kupima afya zao na kati ya hao 103 waligundulika kuwa shinikizo la damu, 62 walikuwa na sukari na 140 wenye uzito uliopindukia.

Nao baadhi ya wananchi waliojitokeza kupima afya zao, Eveline Msanga na Namkunda Mburuja, walisema wamefurahiswa na huduma hizo zinazotolewa kwa kuwa zimefanya watambue afya zao na kanuni bora za afya katika maisha.

HABARI KITAIFA

# Wanafunzi 200 kushiriki maonyesho ya sayansi

**Na Elizabeth Zaya**

WANAFUNZI zaidi ya 200 kutoka katika shule mbalimbali za sekondari nchini, wanatarajia kuonyesha kazi zao za kisayansi katika maonyesho ya wanasayansi chipukizi yanayotarajia kufanyika kwa siku mbili kuanzia Julai 31 hadi Agosti Mosi, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, mwanzilishi mwenza wa Shirika la Wanasayansi Chipukizi(YST), Dk. Gosbert Kamugisha, alisema maonyesho hayo yatawakutanisha wanafunzi wagunduzi na watafiti wa kazi za kiteknolojia.

Alisema kazi hizo ni zile ambazo wameziandaa kwa kipindi cha mwaka mmoja kupitia mpango wa mafunzo ya kisayansi shuleni unaoendeshwa na YST.

Dk. Kamugisha alisema kazi watakazoonyesha wanasayansi hao chipukizi ni katika nyanja za sayansi hususan Kemia, Fizikia na Hesabati, Biolojia na Mazingira pamoja na Sayansi ya Jamii na Teknolojia.

"Ugunduzi wa wanasayansi chipukizi umejikita zaidi katika kutafuta mbinu za kukabiliana na changamoto za maendeleo katika sekta za afya, kilimo na usalama wa chakula, usalama wa mawasiliano na usafirishaji, nishati, elimu, mazingira na mabadiliko ya tabianchi ," alisema Dk. Kamugisha.



Mchuuzi wa ndizi mbivu akisubiri wateja katika Mtaa wa Lindi na Msimbazi, Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kesi ya vigogo Nida yapigwa kalenda

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imepiga kalenda kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Mkurugenzi Mkuu wa zamani wa Mamlaka ya Vitambulisho (Nida), Dickson Maimu na wenzake mpaka Aprili 2, mwaka huu, itakapotajwa tena.

Jana mahakama hiyo ilitaja kesi inayomkabili kigogo huyo wa Nida na wenzake dhidi ya mashtaka 100 ikiwamo kutakatisha fedha na kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 1.16. Hakimu Mkazi Salum Ally alisema kesi hiyo itatajwa tena Aprili 2, mwaka huu, baada ya upande wa Jamhuri kudai wako kwenye hatua za mwisho za kuwasilisha nyaraka Mahakama Kuu.

Wakili wa Serikali, Estarzia Willison, alidai kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba upande wa Jamhuri upo katika hatua za mwisho kukamilisha taratibu za kuwasilisha nyaraka Mahakama ya Kuu.

Mbali na Maimu na Kayombo washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Meneja Biashara wa (NIDA), Aveln Momburi, Mkurugenzi wa Kampuni ya Aste Insurance Brokers, Astery Ndege, Ofisa Usafirishaji, George Ntalima, Mkurugenzi wa Sheria, Sabina Raymond.

# Waziri Lugola akipa neno kitengo cha malalamiko

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola, ametoa wito kwa watumishi wa Wizara hiyo kitengo cha kushughulikia malalamiko ya wananchi, kutekeleza wajibu wao wa kufuatilia na kuyapatia ufumbuzi wa haraka malalamiko wanayopokea.

Lugola aliyasema hayo jijini Dodoma juzi katika kikao kazi kilichoshirikisha watumishi wa kitengo hicho.

Aliwataka wafuatilie malalamiko yanayotolewa na wananchi dhidi ya taasisi zilizopo chini ya Wizara hiyo ambazo ni Jeshi la Polisi, Uhamiaji, Magereza, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

"Hakikisheni malalamiko mnayoletewa mnayapatia ufumbuzi wa haraka bila kufika ngazi ya juu, tekelezeni wajibu wenu kwa ufanisi ili kujenga imani kwa wananchi (walalamikaji).

"Kama wananchi watajiridhisha kuwa kitengo hiki ni msaada mkubwa kwao, mtakuwa mmejijengea uaminifu na kuifanya Wizara ijitegemee kushughulikia malalamiko," alisema.

Lugola alisisitiza umuhimu wa viongozi wanaoshughulikia malalamiko yanayotolewa na wananchi kuchukuliwa hatua kama itabainika wameshindwa kutimiza wajibu wao.

Alisisitiza umuhimu wa kubadili mfumo wa kushughulikia malalamiko akisema yanapofikishwa katika kitengo hicho yachunguzwe hapo hapo wizarani.

"Malalamiko yasirudishwe kwenye taasisi zinazolalamikiwa kama Polisi, Uhamiaji, Magereza, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji pamoja na NIDA...pia walalamikiwa waitwe na kuhojiwa.

Aliongeza kuwa, malalamiko mengine hayapaswi kuchukua muda mrefu ili kutatuliwa, akitolea mfano malalamiko ambayo aliyapokea kwa wananchi na kuyapatia ufumbuzi wa haraka kwenye ziara alizofanya katika mikoa mbalimbali.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Meja Jenerali Jacob Kingu, aliwapongeza watumishi wa kitengo hicho kwa kuyafuatilia malalamiko yanayotolewa na wananchi pamoja na kuyafanyia kazi kwa haraka.

Alisema kitendo cha kupokelewa, kuyafanyia kazi malalamiko ya wananchi ndani ya muda mchache, kitawezekana kama kila mtumishi anayeshughulikia malalamiko atawajibika ipasavyo ili kupunguza mrundikano wa malalamiko yanayotolewa.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Fursa ya kushuka gharama za upimaji ardhi ichangamkiwe

**MOJA** ya mambo ambayo kwa muda mrefu yamekuwa yakiwakwaza wananchi wengi ni gharama kubwa za upimaji wa ardhi. Upimaji ardhi ni jambo muhimu na lenye manufaa kwa kila mmoja kwa sababu ardhi iliyopimwa ina thamani na ni rasilimali muhimu kwa mmiliki.

Ukweli huo unatokana na kwamba ardhi iliyopimwa hata mmiliki anapoamua kuiuza anauzwa kwa bei, hivyo fedha anazozipata anaweza kuzitumia kwa maendeleo na hata akiamua kuziwekeza zinaweza kumwezesha kuanzisha mradi mkubwa.

Aidha, ardhi iliyopimwa inamwezesha mmiliki wake kujiondolea umaskini kwa kuwa anaweza kuitumia kama dhamana kwenye benki na taasisi zingine za kutoa mikopo kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Kadhalika, ardhi iliyopimwa inamfanya mmiliki kuwa na uhakika wa usalama wake kwa kuwa sio rahisi kuvamiwa na kuporwa na wajanja, tofauti na ambayo haijapimwa.

Ni dhahiri kwamba huko nyuma ni kwamba wananchi walikuwa wanashindwa kupima ardhi yao kutokana sababu kadhaa zikiwamo gharama kubwa, urasimu na vitendo vya rushwa vilivyokuwa vinafanywa na baadhi ya watumishi wa umma husan maofisa wa ardhi katika wizara husika na halmashauri.

Hata hivyo, hatua iliyotangazwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ya kushusha gharama za upimaji na urasimishaji ardhi kutoka Sh. 250,000 hadi Sh. 150,000 kuanzia juzi ni ya kupongeza kwa kuwa ni ukombozi kwa wanyonge.

Huko nyuma kwa hakika gharama za upimaji ardhi zilikuwa kubwa kiasi kwamba waliozimudu ni matajiri, hivyo kuwaacha maskini kukaa miaka mingi bila ardhi yao kupimwa.

Baada ya serikali ya awamu ya tano kuingia madarakani, tumeshuhudia jinsi ilivyoweza kusimamia kwa dhati masuala ya ardhi hivyo kero nyingi zilizokuwa zinawakabili wananchi kwa muda mrefu kupatiwa ufumbuzi.

Tumeshuhudia kasi kubwa ya ufumbuzi wa migogoro ya ardhi pamoja na kupunguzwa kwa gharama za urasimishaji na upimaji wa ardhi. Kwa mfano, kabla ya uamuzi wa juzi wa kupunguza gharama hizo hadi Sh. 150,000, serikali ilizishusha hadi Sh. 300,000.

Kadhalika, serikali imeshughulikia uwezeshaji kwa wananchi kupitia ardhi ikiwamo utoaji wa hati za kimila, kupima viwanja na mashamba na kutoa hati kwa wananchi. Hatua hiyo imewawezesha wananchi wengi kuwa na maeneo yaliyopimwa sambamba na kumilikishwa hati.

Kutokana na hatua hiyo, tunaamini sasa kwamba hata makampuni binafsi ya upimaji wa ardhi hayatatumia njia za ujanja kuwapimia ardhi wananchi kwa gharama za juu.


Tunaamini kuwa serikali itadhibiti nyendo hiyo kutokana na kauli ya Waziri Lukuvi juzi ya kuwatahadharisha watumishi wa wizara yake ambao wanamiliki kampuni za upimaji na urasimishaji ardhi kuchagua kufanya kazi serikalini au kutumikia kampuni zao.


Lukuvi alitoa maagizo hayo wakati akizungumza na watumishi wa wizara hiyo na kampuni za upimaji na urasimishaji ardhi jijini Dar es Salaam na kuwaeleza kwamba kazi hiyo imekuwa ikitumia gharama kubwa.

Bila shaka ujanja huo anaijua kutokana na kueleza kuwa ameshusha gharama hizo baada ya kupokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wanaodai kutozwa gharama kubwa wakati wakitaka kupimiwa ardhi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

# Kijiji kilichokosa shule miaka 29 kizaliwe upya

Na Yasmine Protace, Mkuranga

**ELIMU** ni ufunguo wa maisha kwa kila mtu. Lakini, kinachomsaidia mtu kujua kusoma na kuandika, ni pale anapopata fursa ya kusoma shule na akafuatilia masomo kwa hatua.

Kunapokuwapo shule katika sehemu yoyote, kunawawezesha watoto au watu waliokosa elimu kupata elimu inayokomboa maisha yao.

Niseme, bila ya kuwa na msingi wa elimu mtu yoyote, inakuwa vigumu au jamii inashindwa kabisa kufikia malengo binafsi, hata ya kijamii na kitaifa.

Tangu uhuru na zama za kale zaidi, jamii imekuwa ikihamasishwa kuwapeleka watoto wao shule, ili wakapate elimu ambayo itakuwa mkombozi kwa maisha yao sasa na baadaye.

Kuna historia ndefu imeshafanyika katika kuikuza elimu.

Suala la upatikanaji elimu, limekuwa likizingatiwa hata na ngazi za juu zaidi katika uongozi wa nchi, Rais Dk. John Magufuli, alipoingia katika awamu yake ya uongozi wa nchi, alitangaza fursa ya elimu bure

Hapo inamaanisha kuanzia wanafunzi wa msingi, hadi sekondari kidato cha nne. Lengo ni kuwasaidia wasio na uwezo kuwapeleka watoto shule wakasome.

Hatua hiyo imeungwa mkono na jamii, wengi wamehamasika kuwapeleka shule watoto wao. Majibu yakaonekana mapema, wengi wamehamasika kuandikishwaji watoto wao shule, katika maeneo mbalimbali nchini, hali iliyochangia kuongeza udahii kila mwaka.

Pamoja na jitihada hizo za elimu bure, kuna baadhi ya maeneo nchini ni sawa na 'kumpigia mbuzi gitaa' kwa maana ya kuwe nyuma katika upatikanaji huduma hiyo, ambayo imeshafunguliwa milango.

Uhalisia wake unapatikana katika kijiji cha Sangatini wilaya ya Mkuranga, mkoa wa Pwani, ambako wana miaka 29 katika kijiji hicho bila ya kuwa na shule ya msingi hata ya awali.

**Kwa mujibu wa mwenyekiti wa Kijiji hicho, Abdallah Ramadhani Mhando, kijiji chao chenye jumla ya wakazi 309, kilianzishwa mwaka 1990, lakini kinakabiliwa na changamoto nyingi mbali na shule ambazo ni umeme, shule na barabara.**

Ni adha ambayo imewaweka katika mtihani wanakijiji ambao watoto wao wamekuwa 'wakichapa mguu' umbali wa kilomita 14, kwenda kusoma shule za awali na msingi zilizoko Kigamboni jijini Dar es Salaam.

Kutokana na umbali huo, baadhi ya wazazi wameshindwa kuwapeleka watoto wao shule. Baadhi ya wazazi waliozungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, kwamba kuna kila sababu ya kijiji hicho kuwa na shule, kuwakomboa kutoka katika adha hiyo.

Wanaongeza kuwa, watoto wadogo wanalazimika kutembea umbali mrefu kila siku kwenda Kigamboni kusoma hali inayowachosha kiasi cha kushindwa kuwapeleka watoto wao shule.

Kwa mujibu wa mwenyekiti wa Kijiji hicho, Abdallah Ramadhani Mhando, kijiji chao chenye jumla ya wakazi 309, kilianzishwa mwaka 1990, lakini kinakabiliwa na changamoto nyingi mbali na shule ambazo ni umeme, shule na barabara.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Vianzi, Nassoro Chuma, anakiri changamoto tajwa akiongeza lingine la maji.

Chuma anasema, katika suala la shule ya sekondari, wanafunzi wanatembea umbali wa kilomita 14 kwenda kusoma katika Shule ya Sekondari Vianzi. Anaeleza wanavyojipanga ni kwamba, wameishapata fedha Sh. milioni 37 kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari Marogoro, ambako wanafunzi watasoma kutoka vitongoji vya kijiji hicho.

Anaongeza kuwa fedha Sh. milioni 10 zimetolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani kwa ajili ya Ujenzi wa Shule ya Msingi Sangatini, huku katika suala la umeme, kumeanza kuandaliwa nguzo kwa ajili ya baadhi ya vijiji.

Kimsingi, yote tumeyaona na kuyasikia, lakini niseme kikubwa tunahitaji kushuhudia mapya katika kijiji ambacho fursa ya elimu na huduma nyinginezo imebaki kuwa ndoto. Tuanze sasa, tutafika.

## BARUA/MJADALA

### Ziara ya Rais imetufunza

**Mhariri,**

*SIKU chache zilizopita nilikuwa nafuatilia ziara ya Rais Dk. John Magufuli katika mikoa ya Kusini na kisha Nyanda za Juu Kusini.*

*Ni ziara iliyokuwa na fursa alizotoa kwa wananchi kuongea yanayowagusa au kuwasibu. Yaliibua mengi yanayohusiana na kukosekana tija katika miradi ya kiserikali, inayohusu matumizi makubwa ya pesa.*

*Kwa habari nzuri, kuna miradi iliyohusu ujenzi wa stendi, pia maji ambako pale Rais Dk. Magufuli, katika kujumuika na umma mikutanoni, alibaini mambo ambayo hayajakaa sawa na kuanzisha maswali ya papo kwa hapo na kuhitaji majibu ya hapo kwa hapo kutoka kwa wadau husika.*

*Hapo ninataja mifano michache, hasa katika tukio la miradi ya ujenzi wa stendi mjini Njombe, pia mradi wa kuvuta maji yanayotumika katika mji wa Makambako, mkoani Njombe.*

*Ni mjadala ulioibua maelezo yanayogusa mengine na upungufu katika miradi mikubwa inayogusa maisha ya umma.*

*Hata katika mfano wa maji Makambako, ufafanuzi uliibua umma upungufu ulioko katika mamilioni ya pesa yanayotumika katika kuwahudumia.*

*Waliokuwapo na wengine tuliofuatilia kupitia radio na televisheni, tuna ushuhuda wa kutosha kuhusiana na mambo hayo yote.*

*Tuliona maamuzi mazito yaliyofanywa na Rais Dk. Magufuli katika kuweka sawa upungufu wa kijamii ambao ndiyo kilio cha umma, unahitajika kufanyiwe kazi zinazostahili kuweka maisha.*

**Gange Hija,**
**Dar es Salaam.**

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Viwanda zaidi vya mafuta alizeti viongezwe Musoma




**Na Sabato Kasika**

ALIZETI ni miongoni mwa mazao muhimu ya biashara, ambalo kilimo chake kinazidi kuenea mikoa mbalimbali nchini na inawezekana kwa namna moja au nyingine, linachangia kukuza uchumi wa wananchi.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba, mbegu zake hutoa mafuta ya kupikia, wakati makapi yanayotokana na mbegu hizo, ambayo huitwa mashudu, inasemekana ni chakula kizuri kwa ajili ya kulishia mifugo. Kitengo cha Mbegu za Mafuta cha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Uyole, Mbeya, kiliwahi kufafanua kuwa kila hekta moja ya shamba la alizeti, mkulima anaweza kuvuna kati ya magunia matatu hadi matano ya zao hilo.

Upandaji wa zao hilo, unategemea zaidi hali ya hewa ya eneo husika, wakati maeneo yenye mvua nyingi, alizeti huanza kupandwa mwishoni mwa Januari hadi katikati ya Februari, lakini maeneo yenye mvua kidogo, huanza kupandwa mwanzoni mwa Desemba hadi katikati ya Januari.

Aidha, kilo tatu hadi nne za mbegu za alizeti, zinatosha kupanda eneo la ekari moja, hivyo kutokana na hali hiyo, mkulima anashauriwa kupanda mbegu tatu au nne katika kila shimo kwa kuacha nafasi ya sentimita 75 kutoka mstari hadi mstari na sentimita 30 kutoka shimo moja hadi jingine.

Wataalamu nchini wanataja maeneo ambako alizeti inastawi vizuri ni katika mikoa ya Singida, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Kigoma, Rukwa, Katavi na Pwani.

Hayo ni miongoni mwa maeneo ambayo wakulima wake wameanza kuchangamkia kilimo cha alizeti. Sasa Musoma Vijijini, kuna takriban kata zote 21 za eneo wanajishughulisha na kilimo hicho.

Katika misimu mitatu mfululizo, kuanzia wa mwaka 2016/2017 hadi sasa, wakulima wa maeneo hayo wamepokea zaidi ya kilo 9,000 za mbegu za alizeti kutoka kwa mbunge wao, Profesa Sospeter Muhongo.

Alizeti ni zao jipya la biashara katika eneo hilo na inaelezwa inaonyesha kustawi vizuri. Kutokana na hilo, baadhi ya wafanyabiashara wameshawekeza kwenye viwanda vya kukamua mafuta ya zao hilo.

Charles Magoma, ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Musoma Vijijini, anayesema kwa sasa kuna viwanda viwili vya kukamua mafuta ya alizeti, ambavyo vipo katika Vijiji vya Saragana na Kusenyi.

Hapa jambo la msingi ni kwamba kama zao hilo linakubali huko, basi ni vyema viwanda vikaongezwa zaidi kukabiliana na wingi wa mavuno, ili wakulima wasijikute wakihangaika kutafuta sehemu ya kukamulia zao hilo.

Kata 21 ni nyingi sana kwa kuwa kama wakulima wote watakuwa wameitikia viizuri kilimo cha alizeti, halafu hali ya hewa ikawa ni nzuri, maana yake ni kwamba mavuno yatakuwa ni mengi.

Sasa yakiwa mengi wakati viwanda ni viwili tu, vinaweza kuelemewa na mzigo ndio maana nikasema kuna haja ya kuongeza uwekezaji wa viwanda vya kukamua mafuta badala ya kuwa na viwili tu. Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, soko la alizeti lipo ndani ya Musoma Vijijini na mkoa wa Mara kwa jumla. Kama ndivyo ilivyo ni habari njema kwa wakulima wa eneo hilo.

Ninatambua kwamba, zao hilo limeanza kulimwa baada ya kufanyiwa utafiti na wataalamu wa kilimo wa halmashauri, ili kubaini kama zao hilo linakubali katika eneo hilo la Musoma Vijijini na sasa wananchi wanaendelea na kilimo.

Hivyo, kinachotakiwa ni kuongeza idadi ya viwanda na ikiwezekana, kila kata ikawa na kiwanda chake au kata mbili zitegemee kiwanda kimoja, ili kuwapa wakulima uhakika zaidi wa kuuza mavuno yao.

Najua, kuwapo viwanda hivyo viwili ni hatua ya kwanza ya kujivunia. Pia, wawekezaji wengine hawana budi kuangalia fursa ya kuwekeza katika viwanda vingine zaidi vya kukamulia mafuta ya zao hilo. Kwa kuwa Musoma Vijijini, imeshaamua kuwekeza katika kilimo cha alizeti, basi mikakati zaidi iendelee kuandaliwa, ili kuhakikisha zao hilo linapata umaarufu mkubwa.

Vilevile wataalamu wa afya wamekuwa wakipendekeza matumizi ya mafuta ya alizeti katika mapishi, kwa sababu hayana lehemu au (cholesterol), hivyo ni wazi mafuta hayo ni salama.

Kama hali ndio hiyo, basi Watanzania kwa ujumla wao hawana budi kuchangamkia kilimo cha zao hilo, ili kujiongezea kipato. Pia, katika suala la kulinda afya zao kwa kuungia mafuta ya zao hilo katika vyakula.

## KABWELA NA FADHIL MOHAMMED



# Wabunge walia kuminywa

INATOKA UK. 2

cha siasa?

"Lakini hilo limekuwa ni kosa, wenzetu wahariri wa vyombo vya habari wanatakiwa waende wakajieleze. Sasa tunaposifia kwa lipi na tunarudi tunafanya nini?

"Pale tunakuwa hatueleweki, leo vyombo vya habari vinatakiwa vijieleze, kosa lao lipi kwani wanalipwa mishahara kwa kutegemea kazi zao zinavyotoka na kuwajulisha Watanzania kipi kinaendelea katika nchi, sasa Msemaji Mkuu wa Idara ya Habari Maelezo anavitaka vyombo hivyo vikajieleze.

"Lakini cha kusikitisha zaidi na Mheshimiwa Waziri naomba unisikize, yapo mambo kama Mkurugenzi wa Habari Maelezo na wewe waziri mngevitaka baadhi ya vyombo vya habari vijieleze ni muhimu zaidi.

Kwa mfano, kuna vigazeti hapa vigazeti fulani kimoja kinaitwa.... (alitaja jina la gazeti) na kingine kinaitwa ... (alitaja jina la gazeti) na kingine kinaitwa ... (alitaja jina la gazeti), hivi vigazeti kazi yake kubwa ni kuchafua watu, kazi yake kubwa ni kufitinisha watu, kazi yake ni kufitinisha baadhi ya watu.

"Mheshimiwa Mkurugenzi wa Idara ya Habari hajawahi kuviita wala kuwaita wahariri wa magazeti haya akawaambia njoo mjieleze kwa namna mnavyoendelea kuwachafua watu na wapo watu ambao tunawaheshimu sana ndani ya nchi hii mfano Kinana, mtu muhimu kwa nchi yetu anavyochafuliwa na watu hawa, lakini hakuna mkurugezi wala waziri aliyemwita mkurugenzi na mhariri wa gazeti hili mkamwambia namna anavyowachafua watu.

"Na anavyojiamini hadi akaweza kumchafua mtu yeyote, na mtu yeyote katika nchi hii akiamua kumchafua mtu anamchafua, hakuna lolote linalochukuliwa kwake.

Je, (alitaja jina la mkurugenzi wa kampuni ya magazeti) yupo nyuma ya nani? Mimi nilidhani mtu kama huyu akaitwa na kuelekezwa na anachofanya siyo sahihi, akitokea mtu mwingine akaandika katika mtandao anaitwa katika vyombo vingine," Khatibu alisema.

**DEVOTHA MINJA**

Mbunge wa Viti Maalum, Devotha Minja (Chadema), alisema siyo tatizo kuwa na vyombo vingi vya habari, bali tatizo liko kwenye kuviruhusu vifanye kazi yake bila kuingiliwa na dola.

Alisema kukosekana kwa uhuru wa vyombo vya habari kunaanzia ndani ya Ukumbi wa Bunge kutokana na wabunge kutotendewa haki kwa kupewa vipande vya video na sauti ya kile wanachokizungumza ndani ya Bunge.

Alisema kuwa na magazeti mengi au redio nyingi hakuna maana kama vyombo hivyo vya habari havina uhuru katika kujiendesha na kutekeleza majukumu yake.

Devotha pia aliungana na Khatibu kuzungumzia hatua zinazochukuliwa na Maelezo dhidi ya magazeti, akieleza kuwa idara hiyo imegeuka kuwa ni kitanzi kwa waandishi wa habari kwa kuwa kazi yake kubwa kwa sasa kuwataka wajieleze ni kwanini wasifungiwe badala ya kuwaelekeza cha kufanya kuboresha kazi zao.

**JOSEPH MUSUKUMA**

Mbunge wa Geita Vijijini, Joseph Musukuma (CCM), alisema pamoja na mambo mengine, serikali imewatelekeza wasanii wa filamu kwa kutowawekea mazingira mazuri na badala yake wamebaki kuwa ombaomba na kusubiria michango ya kwenye misiba.

**WILLIAM NGELEJA**

Mbunge wa Sengerema, William Ngeleja (CCM), alisema Tanzania inafanya vizuri kwenye sekta ya michezo kwa sasa kutokana na jitihada zinazifanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau.

Alisema hata timu za Bunge zinafanya vizuri zaidi katika michezo kutokana na maandalizi mazuri kabla ya kushiriki mashindano husika.

# Msichana anayesumbuliwa

INATOKA UK. 3

dawa ya Flagyl kwa kuipaka hapo, hivyo nikawa nafanya hivyo," alisema.

Alisema licha ya kuweka unga wa dawa hiyo kwenye kidonda mara baada ya kusafishwa, lakini haikusaidia zaidi kiliendelea kuongezeka ukubwa.

Alisema kutokana na hali ya kimaisha ya nyumbani ilifikia hatua marafiki zake aliosoma nao, walimchangia kiasi kidogo ambacho kilimuwezesha kununua baadhi ya vitu vilivyokuwa vinahitajika kwa ajili ya kukiosha kidonda hicho.

"Matumizi ya unga wa dawa hii haikuwa ushauri wa daktari, kuna mtu alituambia kuwa tukifanya hivyo kidonda kitapona hivyo kila siku nilikuwa nafanya baada ya kuoshwa," alisema na kuongeza:

"Rafiki yangu ambaye nimesoma naye elimu ya sekondari alikuja kunitembea nyumbani na alipoona hali ninayopitia huku familia ikiwa haina fedha za kunitibu, alinishauri nirekodi video fupi ili niombe msaada kwa wasamaria wema mitandaoni ambayo ndiyo iliyomuwezesha kumfikisha hospitali ya Muhimbili," alisema.

Mariam aliishukuru Hospitali ya Muhimbili kwa msaada huo walioutoa kwake kwa kumsafirisha kutoka Singida hadi hospitalini hapo na kumtibia bure.

"Naishukuru sana Hospitali ya Muhimbili kwa msaada walioutoa kwangu Mungu awabariki sana, wananitibia bure, wananihudumia kila kitu hadi chakula," alisema.

Daktari Bingwa Mkuu wa Idara ya Upasuaji Hospitali ya Muhimbili, Ibrahim Mkoma, alisema kwa kawaida kidonda chochote kinachotokea kwenye kovu siyo cha kuchukuliwa kwa wepesi bali mhusika apelekwe hospitali.

Pia alisema mtu huyo akifikishwa hospitalini, wataalamu wasishie kukisafisha bali walichunguze kama ni cha kawaida au saratani.

"Mara nyingi vidonda vinapotokezea kwenye kovu ni saratani na mara nyingi huwa kinaanza kama kiuvimbe alafu baadaye huwa na tabia kinapasuka na unatumia dawa hazisaidii, kadri unavyokisafisha ukikifungua unakuta kimeongezeka. Hivyo hali hiyo ikizidi miezi mitatu ujue hicho siyo kidonda cha kawaida," alisema.

Dk. Mkoma alisema wameshaanza hatua za awali za matibabu baada ya kuona kidonda hicho chenye umri wa miaka mitano.

"Kwa historia Mariam akiwa na umri wa miaka mitano aliungua moto na jeraha lilipona, ndipo miaka mitano iliyopita kikaanza tena. Kutokana na historia ya kidonda hiki mara nyingi kidonda kinapotokea kwenye jeraha sugu tunachukulia kwa tahadhari kwa sababu siyo vya kawaida, kinaweza kikawa cha kawaida ama saratani," alisema.

Alisema utaalam na uzoefu unaonyesha kidonda hicho siyo cha kawaida hivyo wamechukua sampuli ambayo imepelekwa maabara ambayo itatoa majibu kama ni saratani au la.

Alisema mara nyingi aina hiyo ya vidonda huwa ni saratani ambayo hutokea kwenye makovu ya vidonda vilivyotokea muda mrefu uliopita.

# Ofisi za mabati zageuka kivutio

INATOKA UK. 2

wafanyakazi na changamoto zingine zitaonekana si kitu katika utendaji.

"Wizara yetu bado jengo halijakamilika, lakini baada ya agizo la Rais Magufuli tuliweza kujipanga chini ya waziri wetu, Selemani Jafo na kuhamia kwenye mabanda yaliyojengwa kwa mabati na tunaendelea kutoa huduma hapa," alisema.

Aliongeza: "Kama unavyoona hapo ni ofisi zetu na tumeendelea na kutoa huduma kwa watu wanaofika kutafuta huduma, wanaohitaji huduma za Tamisemi wafike katika ofisi hizi watatukuta tupo," alisema.

Naibu Katibu huyo alisema kila siku wanaanzia mipango yao yote ya kazi katika ofisi hizo kabla ya waziri na manaibu wake kuelekea bungeni kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

Aidha, alisema kutokana na kutokuwa na ukumbi katika jengo hilo wanaendelea na kutumia kumbi za majengo yake ya Tamisemi zilizopo katikati ya mji hadi ujenzi utakapokamilika.

Kwa mujibu wa Waziri Jafo, ujenzi wa jengo hilo utakamilika Mei 30, mwaka huu.

Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ambao awali walikuwa hawajakamilisha jengo lao, lakini kwa sasa limekamilika, mmoja wa wafanyakazi wake Innocent Mungi, ambaye alikuwa akitekeleza majukumu yake alisema tayari viongozi wake wamehamia.

"Tumeshahamia huku na tunaendelea na kazi, waziri wetu kahamia na Katibu Mkuu wetu yupo pamoja na watumishi wengine tunachapa kazi, karibu sana," alisema.

Usafiri changamoto

Pamoja na huduma kutolewa na wizara hizo kumekuwapo na changamoto ya usafiri hususani kwa wananchi wanaotaka kufika kwenye eneo hilo.

Tatizo hilo limeonekana ni changamoto kutokana na kulazimika kutumia pikipiki maarufu kama bodaboda kuzifikia wizara hizo.

**Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-**

- **Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=**
- **Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=**
- **Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima**
- **Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku**



## HABARI KITAIFA

# Bil. 1.5/- zatolewa ujenzi hospitali wilaya

**Na Ibrahim Yassin,** MBEYA

SERIKALI imetoa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbeya Vijijini, baada ya Kijiji cha Nyanyala kutoa kiwanja cha ekari 3, huku wananchi wakitoa nguvu kazi zao kuhakikisha ujenzi huo unakamilika haraka.

Kwa sasa wakazi wa Halmashauri ya Mbeya Vijijini wanapata huduma za afya katika Hospitali ya Ifisi inayomilikiwa na Kanisa Katoliki iliyopewa ahadi ya kuwa hospitali teule.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Mwalimu Kisembo, alisema kata yenye vijiji saba imetoa eneo la ekari 31 kwa ajili ya ujenzi huo baada ya kukidhi vigezo vya kuwa na sifa ya kujengwa hospitali.

Alisema majengo 7 yatajengwa, huku kila kijiji kitapewa jengo lake ambapo nguvu ya wananchi iliyothaminishwa ni Sh. milioni 32.5, na kuwa ukichanganya na thamani ya viwanja zinakuwa Sh. milioni 95 ambazo ndizo nguvu za wananchi.

Aliongeza kuwa serikali imewapa maelekezo ya kujenga majengo 7 ambayo ni maabara, jengo la mama na mtoto, jengo la kutunzia dawa, kupumzikia, kufulia, jengo la upasuaji, utawala, X-ray, na kwamba ifikapo Juni 30, mwaka 2020 wataikabidhi Tamisemi ikiwa imekamilika.

"Tuna uhakika tutakamilisha ujenzi huo kwa muda uliopangwa kwa kuwa wananchi wameanza kutumia nguvu kazi zao, wamechimba msingi mita moja na kujaza udongo kwenye vyumba, nguvu ambayo imethaminishwa kwa fedha," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wenzake, Juliana Joseph, alisema kwa muda mrefu walikuwa na ndoto ya kupata hospitali ya serikali ili kutibiwa kwa gharama nafuu.

Alisema serikali imesikiliza kilio chao baada ya kuwapatia fedha hizo kwa ajili ujenzi wa hospitali itakayopunguza msongamano kwa wagonjwa, ambao wamekuwa wakijazana katika Hospitali Teule ya Ifisi iliyopo Mbalizi.

Kukamilika kwa hospitali hiyo kutaifanya Mbeya Vijijini kuwa na hospitali mbili zitakazotoa huduma kwa wananchi hasa waliopo pembezoni zikisaidiana na vituo vya afya vya Ilembo, Ikumbo na Sektaria.



Taka zikiwa zimetelekezwa katika kituo cha daladala cha Shekilango, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Askari FFU wajitolea damu kusaidia jamii

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

KATIKA kukabiliana na upungufu wa damu unaoukabili mkoa wa Kagera na kutishia maisha ya makundi yanayoongezeka kuhitaji kuongezewa damu wakiwamo wajawazito wanaojifungua kwa njia ya upasuaji, askari polisi Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) wamejitolea kuchangia damu.

Askari hao wamejitolea damu kusaidia makundi hayo wakiwamo watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano na majeruhi wa ajali.

Wakizungumza wakati wa zoezi hilo, baadhi ya askari waliozungumza na waandishi wa habari waliwaomba wananchi kujitokeza kwa wingi kujitolea damu, ili kuokoa maisha ya Watanzania wenzao wanaohitaji kuongezewa damu.

Mmoja wa askari hao, Juma Ramadhan, alisema ameguswa na tatizo la watu wanaopoteza maisha kwa sababu ya kukosa damu, na kuwaomba askari wenzake kujitokeza kuchangia damu ili kunusuru maisha ya wananchi wenzao.

Askari mwingine, Slyvester Mazanza, alisema kuwa yeye kama askari anayelinda raia na mali zake hapendi kusikia raia apotee kwa kukosa damu wakati ana uwezo wa kujitolea damu.

"Kuna ndugu zetu kama wajawazito ambao wanapoteza damu nyingi wakati wa kujifungua na watoto, wanahitaji kuongezewa damu, sisi kama askari tumejisikia fahari kushiriki katika zoezi hili," alisema. Sajenti Charles Fabian alisema ni vema askari kuwa mfano kuchangia damu na kuwa wao wako tayari kuchangia muda wowote wanapohitajika kufanya hivyo, ili kuhakikisha afya za Watanzania ziko salama.

Kwa upande wake, kiongozi mshauri wa timu ya damu salama mkoa wa Kagera, Amos Bashweka, aliyeongoza zoezi hilo, alisema mkoa unakabiliwa na upungufu wa wastani wa chupa 200 za damu kwa mwezi, kati ya wastani wa chupa 1,000 zinazohitajika.

Bashweka alisema katika zoezi hilo wamefanikiwa kukusanya chupa 50 za damu na kuwa zitasaidia kukabiliana na upungufu wa damu katika hospitali zao.

## ATAPE yawekeza bil. 1/- miradi ya maendeleo

**Na Happy Severine,** BARIADI

CHAMA cha Wanataaluma na Wajasiriamali wa Kanisa la Waadventista Wasabato (ATAPE), kimewekeza Sh. bil 1.039 katika miradi mikubwa mitano ya maendeleo na kutoa ajira zisizo rasmi kwa Watanzania kwa zaidi ya asilimia 90.

Chama hicho chenye wanachama zaidi ya 1,500 nchini kwa umoja wao kimefanikiwa kuwekeza katika miradi ya uinjilisti, ujasiriamali, elimu, maji na afya.

Akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano wa kitaifa wa 20 wa chama hicho, unaofanyika kitaifa mkoani Simiyu, Mwenyekiti wa chama hicho taifa, Freddie Maneto, alisema kuwa chama hicho kimepiga hatua kubwa kiuchumi kwa kuwekeza kiasi hicho cha fedha.

"Tunaposherehekea miaka 20 ya chama chetu cha ATAPE, tunajivunia mambo mengi makubwa tuliyoyafanya na kufanikiwa...tumeweza kuwekeza kiasi cha Sh. bil. 1.039 fedha za miradi toka kwa wanachama wenyewe...na kufanya miradi ya kijamii kama kilimo, ujasiriamali kufanikiwa kwa kiasi kikubwa," alisema Manento.

Alisema mbali na miradi hiyo, pia wanatarajia kuanzisha miradi mingine ya malazi (hosteli) ili kutoa huduma zaidi kwa jamii.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, alisema kupitia mkutano huo wa ATAPE utasaidia mkoa wake kukuza kipato kupitia shughuli mbalimbali zitakazofanyika kwa kipindi chote cha mkutano huo.

Mtaka aliongeza kuwa, wakazi wa Simiyu ifikie wakati wa kuchangamkia fursa mbalimbali za kibiashara zilizopo mkoani humo kwa kuwa mkoa kwa sasa unahitaji kuwekeza zaidi katika shughuli za kibiashara.

John Bubinza, mjasiriamali wa Mjini Bariadi, alisema wanashukuru uwapo wa mkutano huo kwa kuwa wanajipatia kipato kupitia shughuli zao wanazofanya ndani ya mkutano huo.

# Sababu Mirembe kujengwa Dodoma

BUNGE limeelezwa kuwa kujengwa kwa Hospitali ya Mirembe hakumaanishi kuwa wagonjwa wengi wa akili wapo jijini Dodoma, bali ni kutokana na uwapo wa gereza kubwa la Isanga.

Majibu hayo yalitolewa na Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, baada ya Spika Job Ndugai kuhoji sababu za serikali kujenga hospitali hiyo ya magonjwa ya akili Dodoma.

Spika Ndugai alisema nchi nzima imejengwa miradi ya maana likiwamo Jiji la Dar es Salaam, lakini Dodoma wakaletewa hospitali hiyo.

Dk. Ndugulile alisema sio kwamba wagonjwa wengi wapo hapa jijini Dodoma, bali walijenga hospitali hiyo kutokana na uwapo wa gereza kubwa la wafungwa Isanga. Alisema gereza hilo, wafungwa wake wengi ni wenye kesi za mauaji, hivyo hospitali hiyo hutumika kujua kama afya zao za akili zipo vizuri au laa kutokana na matukio waliyofanya.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Njombe Mjini (CCM), Edward Mwalongo, alitaka kujua kama serikali kuwahudumia wagonjwa wa akili wanaozurura mitaani katika masuala ya matibabu, mavazi na makazi.

Dk. Ndugulile alisema jamii inatakiwa kuacha kunyanyapaa wagonjwa wa akili badala yake wawafikishe kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwa kuwa ugonjwa wa akili hauna uhusiano na imani za kishirikina.

"Jamii inapaswa kuibua watu wanaoonekana kuwa na dalili za ugonjwa wa akili na kuwapeleka kwenye vituo vya afya ili wapatiwe matibabu kwa kuwa huduma hiyo ipo na inatolewa bila gharama yoyote," alisema.

Alieleza kuwa magonjwa ya akili yanatibika na kutoa rai kwa jamii waache kuwanyanyapaa wagonjwa hao badala yake wawafikishe kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwa kuwa hauna uhusiano na imani za kishirikina.

Naibu Waziri huyo alisema pamoja na kuongezeka kwa wagonjwa wa akili wanaorandaranda barabarani, Sheria ya Afya ya Akili ya Mwaka 2008 inawataka ndugu na jamii kuibua wagonjwa wa akili na kuwapelekea vituo vya kutolea huduma ili wapatiwe matibabu. "Wagonjwa wakishapata nafuu huruhusiwa kwenda kukaa na familia zao na kwenye jamii wanazotoka na jukumu la kwanza la kulinda afya ya jamii huanzia katika ngazi za familia, lakini jamii zimekuwa zikiwanyanyapaa, kuwabagua na kuwatenga wagonjwa wa akili kunakosababisha wagonjwa hao kurandaranda,"alisema.

Alifafanua kuwa kwa mujibu wa sheria hiyo ya afya ya akili sehemu ya tatu kifungu cha sheria namba (9) kifungu kidogo (1-3) imeeleza wazawazi kuwa ofisa polisi, usalama, ustawi wa jamii ngazi za wilaya, pamoja na viongozi wa dini, afisa mtendaji wa kata, kijiji wana jukumu la kumfikisha kwenye sehemu ya uchunguzi wa magonjwa ya akili.

# TPA, ZPC zaendelea kushirikiana

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari (TPA) na Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC), zimeendelea kubadilishana utaalamu na kushirikiana katika kutoa huduma za bandari nchini hususan katika uongozaji meli kutoka nje ya nchi.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Magogoni (CUF), Dk. Suleiman Ally Yussuf. Katika swali lake alihoji Serikali ya Muungano inaungaje mkono nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kujenga bandari kubwa.

Akijibu, Sima alisema kwa mujibu wa Sheria ya Bunge namba 17 ya mwaka 2004 majukumu ya TPA ni kuendeleza bandari, kuendesha shughuli za bandari, kutangaza huduma za bandari na kushirikisha na kusimamia sekta binafsi katika uendelezaji na uendeshaji wa bandari.

Aidha, alisema ZPC ilianzishwa kwa Sheria ya Bandari ya mwaka 1997 na ina majukumu ya kuendeleza Bandari, kuendesha shughuli za bandari na kutangaza huduma za bandari ndani na nje ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Pia, alisema Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, nyongeza ya kwanza imeorodhesha mambo ya muungano, ambapo kipengele cha 11 katika orodha ya mambo ya Muungano kinahusu bandari, mambo yanayohusika na usafiri wa anga, posta na simu.

Kwa kuzingatia maelezo hayo, Naibu Waziri huyo alisema serikali ya Tanzania na Zanzibar zimeendelea kushirikiana katika masuala mbalimbali ya uendelezaji wa bandari nchini.

"Ushirikiano huo umedhihirika zaidi katika kupanga miradi ya vipaumbele na kutafuta fedha za uendelezaji wa miradi hiyo kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na washirika wa maendeleo," alisema.

Sima alisisitiza TPA na ZPC zimeendelea kubadilishana utaalamu na pia wataendelea kuboresha ushirikiano kupitia vikao vya mara kwa mara vya sekta ya uchukuzi.

"Kwa kuzingatia maelezo hayo, Serikali ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikiunga mkono nia ya serikali ya Zanzibar ya kujenga bandari kubwa ili kuimarisha miundombinu na huduma za bandari nchini," alisema.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Mbunge wa Mtwara Mjini (CUF), Maftah Nachuma, katika viwanja vya Bunge jijini Dodoma juzi. **PICHA: OWM**

# Wenye ulemavu wa macho wakumbukwa uchaguzi ujao

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira), Anthony Mvaunde, amesema katika uchaguzi ujao ngazi zote Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) itaandaa karatasi maalum za kupiga kura kwa kutumia mfumo wa nukta nundu kwa ajili ya walemavu wa macho.

Mavunde alitoa kauli hiyo alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Susan Mgonukulima, ambaye alisema walemavu wa macho wamekosa haki ya kuchagua viongozi wanaowataka kutokana na kusaidiwa kupiga kura na watu wengine ambao wanaweza kuwapigia kura kinyume cha ridhaa zao kwenda kwa wagombea ambao si chaguo lao.

"Serikali iko tayari kuchapisha karatasi maalum za kupigia kura kwa kutumia mfumo wa nukta nundu maalum kwa ajili ya walemavu wa macho?" Alihoji.

Akijibu, Mavunde alisema katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, NEC iliandaa karatasi maalum za kupigia kura kwa mfumo wa nukta nundu kwa ajili ya uchaguzi wa Rais pekee.

"Kifungu cha 61(3)(b) cha sheria ya Taifa ya Uchaguzi sura ya 343, na kifungu cha 62(h) cha sheria ya uchaguzi wa serikali za mitaa sura ya 292 vinafafanua kuwa ikiwa mpigakura ni mlemavu wa macho au ana ulemavu wa viungo (mfano mikono) au hawezi kusoma na kuandika anaweza kuchagua mtu anayemwamini amsaidie kupiga kura," alisema.

Alisema mtu huyo anapaswa asiwe msimamizi wa kituo cha kupiga kura, msimamizi msaidizi wa kituo au wakala wa chama cha siasa.

Mavunde alisema kanuni ya 53 ya kanuni za uchaguzi wa Rais na wabunge za mwaka 2015 na kanuni ya 46 ya kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa (madiwani) zimewekewa utaratibu kuwa iwapo mpigakura mwenye ulemavu wa macho atoomba kupewa karatasi ya kupiga kura ya nukta nundu.

Kadhalika, alisema msimamizi anapaswa kumpatia mpigakura karatasi hiyo ili aweze kupiga kura, hivyo katika chaguzi ujao watatumia mfumo huo kwa ngazi zote za uchaguzi.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA




Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro (kushoto), akigawa vitambulisho vya machinga katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo, mkoani Arusha jana, baada ya kufanya ziara ya kushtukiza kuangalia zoezi la ugawaji wa vitambulisho hivyo na kutoridhishwa nalo. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Hospitali yalia ukosefu CT Scan, vyumba vya upasuaji

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

HOSPITALI ya Mkoa ya Arusha ya Mount Meru ina ukosefu wa mashine ya upigaji picha kimatibabu (CT Scan) na uhaba wa vyumba vya upasuaji kulingana na idadi kubwa ya wagonjwa.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Shafii Msechu, alisema hayo wakati akizungumza katika hafla ya kupokea msaada wa mablanketi 100 na mashuka 115 yenye thamani ya Sh. milioni 3.5.

Msaada huo ulitolewa na Shirika la Compassion International Tanzania kwa kushirikiana na ushirika wenza wa makanisa ya kiinjili Arusha katika kuadhimisha miaka 20 ya huduma hiyo.

Alisema hivi sasa hospitali hiyo ina vyumba viwili tu vya upasuaji ambavyo ni vya zamani na ni vidogo ikilinganishwa na idadi kubwa ya wagonjwa iliyopo.

Aidha, aliomba wadau mbalimbali kujitokeza waweze kuhudumia wateja wengi na kwa muda mfupi.

Alitaja changamoto nyingine ni CT Scan, katika hospitali hiyo.

Alisema kutokana na ukosefu wa mashine hiyo, wagonjwa wao wanalazimika kwenda kupata huduma hiyo katika hospitali binafsi.

"Tunashukuru kwa msaada huu wa mablanketi na mashuka kwa kuwa umekuja muda mwafaka ambao tuna uhitaji mkubwa wa vifaa hivyo kulingana na idadi kubwa ya wagonjwa wanaofika hapa kila siku.

Naye Mkurugenzi wa Kituo cha KKKT-TPRI kutoka Shirika la Compassion, Evaline Naimani, alisema katika kuadhimisha miaka 20 ya kituo hicho wameona ni vizuri wasaidie hospitali hiyo mahitaji mbalimbali na kujitolea damu kwa ajili ya kusaidia wagonjwa wenye mahitaji hayo wanaofika kupata huduma.

Alisema katika kuadhimisha miaka 20 ya kituo hicho wamekutanisha vijana kutoka vituo 27 vinavyohudumia vijana hao ndani ya Jiji la Arusha.

"Katika kuadhimisha miaka 30 tunashiriki shughuli za kijamii ambapo kuna makundi mengine yameenda kutembelea vituo vya watoto yatima, huku sisi tukichangia damu, ambapo zaidi ya watu 30 watachangia damu lengo likiwa ni kusaidia kuokoa majeruhi wanaoletwa hapa pamoja na wanawake wajawazito wanaohitajika kuongezewa damu," alisema.

Naye Katibu Tawala Msaidizi, Utawala na Rasilimali, David Lyamongi, akizungumza kwa niaba ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, alisema kitendo kilichofanywa na shirika hilo kinapaswa kuigwa na jamii kwa kuwa wamefanya jambo ambalo litakumbukwa na jamii hasa katika zoezi la kuchangia damu pamoja na utoaji wa msaada wa mashuka na mablanketi.

"Ni vizuri tukawajengea vijana wetu utamaduni wa kuchangia damu mara kwa mara ili kuwa na damu ya kutosha na kuwahudumia watu mbalimbali wenye mahitaji ya haraka," alisema.

Mmoja wa wachangiaji damu katika zoezi hilo, Zephania Megiroo, alisema kuna umuhimu mkubwa wa kuwapo kwa elimu ya uhamasishaji wa kuchangia damu kuanzia ngazi za chini hasa katika shule za msingi na sekondari ili waweze kujua umuhimu wake wakiwa tangu wadogo.

# Mahakama ya Afrika kuteta na Rais Buhari

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

UJUMBE wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (AfCHPR), unatarajia kutembelea mahakama ya Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (Ecowas), Aprili 29 hadi Mei 4, mwaka huu, ambapo pia utaonana na Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari.

Kwa mujibu wa msajili wa AfCHPR, Dk. Robert Eno, ziara hiyo inafuatia ujumbe wa mahakama ya ECOWAS uliofanya ziara kama hiyo Mahakama ya Afrika, jijini Arusha, Februari, mwaka huu, ambapo makubaliano mbalimbali ya mikataba ilitiwa saini.

Kwa mujibu wa Rais wa Mahakama ya Afrika, Jaji Sylvain Ore, ambaye ataongoza ujumbe huo, alisema, ziara hiyo itasaidia kubadilishana uzoefu kati ya mahakama hizo.

Aidha, aliongeza ziara hiyo itasaidia kuimarisha ushirikiano na mahakama za kikanda barani Afrika.

Ujumbe huo utakaohusisha majaji watatu na maofisa waandamizi wa mahakama hiyo unatarajiwa kuonana na Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari na kuonana na maofisa wengine wa ngazi ya juu katika Wizara za Mambo ya Nje na Sheria.

Pia ujumbe huo utafanya mazungumzo na Chama cha Wanasheria cha Nigeria, mashirika yasiyo ya kiserikali na vyama vya kiraia.

Mahakama ya Afrika ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 1 ya Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu ili kutekeleza majukumu ya Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu katika kulinda haki za binadamu.

# Wanawake wajikwamua kwa kunenepesha ng'ombe

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

WANAWAKE katika makundi wilayani Longido, wameweza kununua mifugo na kuinenepesha, hali ambayo imesaidia kuwainua kiuchumi.

Baadhi ya wanawake waliozungumza na Nipashe jana, walisema wamejikwamua kiuchumi kutokana na msaada walioupata kupitia Shirika la PCI International la Marekani.

Walisema shirika hilo limewawezesha kupata elimu ya ujasiriamali na mikopo katika makundi.

Akizungumza na Nipashe, mkazi wa Kata ya Oorbomba, Rahel Laizer, alisema awali wanawake wa jamii ya wafugaji ya Wamasai hawakuwa na elimu hiyo lakini sasa wameipata.

"Tuliishia kuchoma mkaa ili kuendesha familia, lakini sasa tumeweza kupata elimu ya kunenepesha ng'ombe na kufanya ujasiriamali wa aina tofauti.

"Lakini baada ya Shirika la PCI kuingia wilayani hapa limebadilisha maisha ya wanawake kwa kuwezesha vikundi vya kuweka na kukopa na kupitia makundi hayo, tumesomesha watoto na kujenga nyumba bora zilizoezekwa mabati badala ya nyasi," alisema.

Aidha, alisema changamoto kubwa inayowakabili ni umbali wa wana vikundi na mwezeshaji wa elimu ngazi ya jamii, hivyo wanagharamika kusafiri kwa pikipiki na kutumia pesa nyingi zaidi katika safari.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ken Ole Moloimet, aliomba shirika hilo kuendelea kubaki wilayani hapo, kwa kuwa wameonekana kuwa wakombozi wakubwa kwa jamii hiyo, hususani kwa upande wa wanawake.

Alidai kuna kata zenye uhitaji wa elimu na uwezeshwaji huo, na kuwataka kuhakikisha wanawafikia na kata hizo ambazo hazikubahatika kupata mradi huu.

Mkurugenzi wa Shirika la PCI, Nick Ford, alisema mkataba wao ndani ya Wilaya ya Longido utamalizika Septemba, mwaka huu, lakini wataangalia kama wataweza kuendelea kubaki kufanya kazi na halmashauri hiyo.

Alieleza lengo kubwa la PCI ni kuhakikisha wanamnyanyua mwanamke kiuchumi ili aweze kuepukana na umaskini, njaa na maradhi.

Alifafanua PCI ilianza kufanya kazi nchini mwaka 2008, ikitekeleza mradi wa maji salama ulionufaisha wananchi takribani 33,000 katika baadhi ya vijiji mkoani Manyara.

Alidai tangu muda huo, shirika hilo limetanuka na kujikita kupitia programu yake ya chakula shuleni inayofadhiliwa na Wizara ya Kilimo ya Marekani (USA).

Alidai kupitia mradi huo wa chakula shuleni, imeongeza idadi ya wanafunzi walioandikishwa na wanaohudhuria shuleni kwa wingi katika Mkoa wa Mara. Aidha, alisema katika Mkoa wa Arusha wanafanya kazi zao Wilaya ya Longido na Monduli katika kuwawezesha wanawake mikopo na kujiinua kiuchumi.

Hata hivyo, kati ya kata 18 za Wilaya ya Longido wamefanikiwa kuwawezesha wanawake katika kata nne ambazo ni Orbomba, Engikaret, Sinya na Tingatinga.





# Watahadharishwa umakini miundombinu ya Tanesco

**Na Paul William,** MOSHI

WANANCHI wametahadharishwa kufanya biashara chini ya miundombinu ya umeme hasa katika kipindi hiki cha mvua ili kuepuka madhara mbalimbali yanayoweza kuwapata.

Rai hiyo imetolewa jana na Meneja wa Shirika la Umeme nchini (Tanesco), Mkoa wa Kilimanjaro, Mahawa Mkaka, wakati alipozungumza na gazeti hili ofisini kwake ambapo alisema kuwa vitendo vya ufanyaji wa biashara chini ya miundombinu ya umeme inaweza kuhatarisha maisha yao.

Mkaka alisema kuwa kipindi hiki cha mvua miundombinu imekuwa ikiharibika kutokana na upepo mkali zikiendana na radi, ambapo na kwamba ni hatari wananchi wakiendelea kufanya biashara chini ya miundombinu hiyo hasa chini ya transfoma.

Alisema kuwa ni jukumu la wazazi kuangalia watoto wao, kwa kuwa mvua zinazoendelea kunyesha zinasababisha madhara kwa kuanguka kwa nguzo pamoja na kukatika kwa nyaya za umeme kutokana na kuangukiwa na miti.

Meneja huyo alisema kuwa kutokana na madhara hayo ni vyema wananchi wakajijengea tabia ya kuvaa viatu pamoja na kuepuka kukanyaga maji ovyo, kwa kuwa umeme unasafiri kwa kasi sana ndani ya maji.

"Nawasihi sana wananchi kuepukana na kupigwa na shoti ni vyema basi wakachukua taadhari kwa kuvaa viatu, lakini pia waepuke kukanyaga maji ovyo kwani ni hatari sana endapo utakuta nyaya imekatika na kugusa maji kwa sababu umeme huwa na tabia ya kutembea na maji," alisema Mkaka.

Alitoa wito kwa wananchi kuchukua tahadhari pindi panapotokea tatizo lolote linalohusu Tanesco na kuwataka kutogusa nyaya zilizoanguka chini na badala yake watoe taarifa ofisini kwao ili kuepuka madhara makubwa ikiwamo vifo.

Kwa upande wake, Ofisa Uhusiano wa shirika hilo, Mkoa wa Kilimanjaro, Samwel Mandari, aliwataka wananchi kuepuka kufanya biashara au kilimo chini ya miundombinu ya umeme hasa katika kipindi hiki cha mvua kwa kuwa ni hatari kwa maisha yao.

Mandari alisema kuwa, shirika hilo halipendi kuona wananchi wakiathirika kutokana na umeme, na kuwataka kuwa wazalendo na shirika lao kwa kuepuka kufanya shughuli zozote za kijamii chini ya miundombinu ya umeme.

Aidha, Mandari alisema kuwa kwa sasa wanaendelea na operesheni maalum ya kukata miti iliyopo karibu na miundombinu ya umeme ili kuepuka madhara mbalimbali ikiwamo miti hiyo kuangukia nguzo na nyaya za umeme.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, akifafanua umuhimu wa kuwa na Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi za serikali za mitaa wakati wa mafunzo kwa Kamati ya Usimamizi wa Maafa ya Mkoa huo, jijini Mwanza juzi. Kulia ni Mkurugenzi Idara ya Uratibu wa Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu, Jimmy Matamwe. **PICHA: OWM**

# Jeshi la Polisi laweka wazi utendaji wa askari wake

**Mary Mosha na Paul William,** MOSHI

JESHI la Polisi mkoani Kilimanjaro, limesema kitendo cha askari wake, kukaa nje ya kambi kumechangia kuwapo kwa utendaji usiofuata maadili kwa baadhi yao.

Hayo yamesemwa na Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Hamis Issah, wakati akikabidhiwa mifuko 200 ya saruji kutoka kiwanda cha saruji cha Moshi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba sita za watumishi hao.

Alisema kuwa mpaka sasa zaidi ya askari 400 wanakaa nje ya kambi za polisi na hii ni kutokana na uhaba wa nyumba unaolikabili jeshi hilo na kukwamisha utendaji wa kazi usiofuata maadili ya kazi na kusababisha kuangushiwa lawama kila mara.

Alisema kuwa kutokana na changamoto hiyo serikali ya awamu ya tano, chini ya Rais Dk. John Magufuli imeonyesha dhamira ya kuhakikisha inajenga makazi ya askari, ambapo kwa Mkoa wa Kilimanjaro, serikali imetoa Sh. milioni 150 kwa ajili ya kujenga nyumba 6 zinazotarajiwa kukamilika Juni 30, mwaka huu.

Kamanda huyo alibainisha kuwa, mpaka sasa wameshapokea misaada ya vitu mbalimbali kutoka kwa wasamaria wema kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizo sita, ambapo misaada hiyo inagharimu shilingi milioni 11.

Akipokea msaada huo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, aliwaomba wadau waishio ndani na nje ya mkoa huo kuungana kuhakikisha wanajenga nyumba hizo ili fedha iliyotolewa na serikali itumike katika kuzimalizia nyumba hizo.

"Ikiwa tutashirikiana kwa pamoja kazi hii ni nyepesi na itakamilika kwa wakati uliokusudiwa, hivyo kutokana na umuhimu wa Jeshi la Polisi tuungane kwa pamoja katika kumalizia nyumba hizi na kujenga nyingine nyingi zaidi," alisema.

Alimtaka Kamanda Issah kukaa na makandarasi kuangalia gharama zinazoweza kutumika ikiwa majengo hayo yatakwenda juu (ghorofa) kutokana na uhaba wa eneo uliopo mkoani hapa.

Katika hatua nyingine, Mgwira aliomba wanawake kutenga siku moja ya kimkoa na kufika eneo hilo linalomilikiwa na polisi kupanda miti kuzunguka eneo leo ikiwa ni njia moja wapo ya kutunza mazingira ya eneo hilo.

## Waomba polisi kusaka pombe ya gongo

**Na Mary Mosha,** ROMBO

WANANCHI wilayani Rombo mkoani Kilimanjaro, wameliomba Jeshi la Polisi kubadilisha mbinu za kukabiliana na watengenezaji, wauzaji na wanywaji wa pombe aina ya gongo ili kunusuru jamii kutokana na madhara yanatokanyo na unywaji huo.

Hayo yalisemwa jana wakati wakizungumza na Nipashe katika kijiji cha Makiidi, ambapo Erinest Masawe, alisema, kuwa licha ya serikali kujitahidi kutokomeza gongo, lakini bado tatizo ni kubwa.

Elinasari Makata, alisema ipo haja ya polisi kubadili mbinu za kuwakamata watengenezaji na wauzaji wa gongo kwa kuvaa nguo za kiraia pamoja na magari binafsi ili wahusika wasiweze kuwajua.

"Hali ya unywaji wa gongo katika Wilaya ya Rombo bado ni kubwa na polisi hawawezi kulifuatilia hili kwa urahisi kwa kuwa mara nyingi wanapofika eneo la tukio wanakuja kwa magari na wamevalia sare hali inayowafanya wahalifu kutoroka wanaposikia mingurumo yagari," alisema.

"Kwa sasa wauzaji wanatumia mbinu ya kumuuzia mtu na kisha kwenda mbali na wao kwa ajili ya kunywa ambapo wanaficha kwenye nguo, unaweza ukakutana naye na usione kama wamebeba kitu.

Dismas Mrema, alishauri polisi kuhakikisha maeneo yanayopika gongo wawakamate watendaji wa vijiji na vitongoji kwa kuwa walipaswa kuwa wa kwanza kutoa taarifa ya biashara hiyo kutokana na wanaofanya biashara hiyo wanafahamika.

"Wako baadhi ya watengenezaji wa gongo wanaodai kuwa wamepewa kibali cha kutengeneza... hatujui, lakini tunaomba mamlaka husika kufuatilia chini ya ulinzi mkali ili kufahamu uhalali wa vibali walivyonavyo," alisema Mrema.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Agnes Hokororo, alikiri kuwapo kwa matukio kama hayo katika wilaya yake na kusema kuwa tayari jitihada za makusudi zimechukuliwa ikiwamo operesheni maalumu ya ukamataji wauzaji wa gongo na watumiaji, ili kuhakikisha tatizo la gongo katika wilaya hiyo linatokomezwa.

Alisema kwa kipindi cha mwezi Machi hadi Aprili, wamekamata lita 314 za gongo na watuhumiwa zaidi ya 30 ambao wanatarajiwa kufikishwa mahakamani wakati wowote.

"Operesheni hii ni endelevu, tutaendelea kuwakamata watengenezaji wa gongo na wanywaji wote hata wakitumia mbinu mbali mbali bado hatutawaacha na tutahakikisha tatizo la pombe Rombo linabakia kuwa historia," alisema Mkuu wa Wilaya.


Ukurasa 19

Don Bosco yafungua mlango wa pili wa ofisi kupitia teknolojia


Ukurasa 14

Hali ya hewa ilivyotoa darasa kukabili mtikisiko uchumi



## Bosi Volkswagen kortini, 'akiteleza' jela miaka 10

Ukurasa 15

BUFE
Ijumaa Aprili 19, 2019
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



# MTIHANI JINSIA MASOKO YA SHINYANGA

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KADRI miaka inavyoenda, kuna mabadiliko makubwa yanaendelea nchini katika mustakabali wa uchumi ukipiga hatua kubwa.

Hapo katika sekta ya fedha, kuna mageuzi makubwa yanayoshuhudiwa katika sekta ya fedha na hasa teknolojia ya mawasiliano ya habari, ikijikita zaidi katika matumizi ya simu za mkononi. Jamii inafikiwa kila kona na hasa katika maeneo ambayo huduma za kibenki hayajafikiwa.

Kadri kunavyoshuhudiwa mageuzi hayo, kila asasi na hasa benki na kampuni za simu ambazo sasa zimeibuka kuwa mdau mkubwa wa biashara za fedha, zimepiga hatua kubwa.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

## Habari katika picha


Ukurasa 17

KIUCHUMI ZAIDI Ukurasa 19

Takwimu za Biashara Ukurasa 20

Muhtasari wa Soko

**Biashara**

Jumla ya Mauzo (bln) 22,136.24

| | |
|---|---|
| Mauzo | 109,584,255.00 |
| Hisa | 58,317 |

**Kielezo**

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 4,207.58 | +0.00 |
| DSEI | 2,296.50 | -37.11 |

**ZILIZOPANDA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| KA | 180 | -2.70% |
| JHL | 9,500 | +1.06% |
| SWIS | 3,760 | +7.43% |
| EABL | 5,320 | -1.66% |

**ZILIZOSHUKA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| TCCL | 1,200 | -11.76% |
| ACA | 5,550 | -2.63% |
| NMB | 1400 | -1.41% |
| NMG | 2,510 | -1.57% |
| KCB | 840 | +2.44% |

UCHUMI

JICHO TOKA MISSENYI

# Hali ya hewa ilivyotoa dara kukabili mtikisiko uchumi

• Waathirika wasimulia, Ofisa Kilimo anena • Uchumi mlo: Wa kwa nusu hitaji • Mtoto anayepungua uzito apewa upendeleo

**Na Lilian Lugakingira,**

**aliyekuwa Missenyi**



Abubakari Mohamed, mkulima wa kitongoji cha Kilimilile katika Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, akiwa shambani mwake.

MABADILIKO ya hali ya hewa yaliyosababisha ukame katika baadhi ya maeneo ya mkoa wa Kagera mwaka 2017, yalisababisha wakazi wa kijiji Kilimilile katika Kata ya Kilimilile wilayani Missenyi, kula maembe na mafenesi kunusuru maisha yao.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kilimilile, Iss-haka Yunusu, anasema wakati wa ukame, mbali na mazao kukauka, pia mifugo kama ng'ombe na mbuzi ilikufa kwa kukosa malisho.

"Mazao yaliyokauka ni mihogo, mahindi, migomba, mibuni na mazao mengine. Hiyo ilisababisha uchumi wa wananchi kuyumba na wakakosa chakula," anasema Yunusu.

Pia, anasema wananchi waliokuwa na mifugo walilazimika kuiuza ili kupata fedha za kwenda 'kuhemea'chakula, huku wasio na mifugo wakihangaika kutafuta vibarua walipwe pesa au mbadala wa chakula.

Anasema, kwa sasa wamejipanga na mikakati ya kuanza kulima hasa kwa mazao yanayokomaa haraka, vikiwamo viazi mviringo, viazi vitamu ili wapate chakula walau kidogo.

"Naitisha mikutano mara kwa mara katika kitongoji changu. Katika mkutano wa awali, tuliweka mikakati kila mwananchi alime mazao yanayokomaa haraka na tunakwenda kukagua katika kila familia, ili kuona utekelezaji wake," anasema.

Mwenyekiti huyo anasema, kila mwananchi anapaswa kulima kuanzia kiwango cha nusu ekari ya shamba, kwa kila mazao yaliyoainishwa na kuwa anaridhishwa na mwitikio wa wananchi wake.

> **"Wakulima waliozingatia ushauri wa wataalamu waling'oa na kupanda upya na sasa mazao yao yamestawi vizuri.**

**OFISA KILIMO**

Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Missenyi, Tapita Solomon, anasema hali ya hewa ya mwezi Januari mwaka huu, imekuwa na mabadiliko, kutokana na kutozoeleka mvua kunyesha katika kipindi hicho, kwani mkoa wa Kagera una misimu miwili ya mvua ambayo ni vuli na masika.

Solomon anasema, mvua za vuli huanza kunyesha kila mwezi Agosti hadi Desemba na msimu wa masika upandaji wake huanzia mwishoni mwa mwezi Februari hadi Machi.

Ushauri wake ni kwamba, wataalamu wenzake wote wa kilimo na wananchi wakubali kubadilika kwenda sambamba msimu wa mvua unapobadilika.

"Kila mtu kwa nafasi yake akubali kubadilika na wananchi wakubali kupokea ushauri na kuufanyia kazi ili kuepuka athari," anasema.

Solomon anatoa mfano kuwa Septemba mwaka jana hali ya hewa ilibadilika na mvua zikachelewa kunyesha hadi mwezi Novemba, hivyo walichokifanya ni kuwasisitiza wakulima waliopanda mazao yaliyonyauka, wayang'oe na kupanda upya.

"Wakulima waliozingatia ushauri wa wataalamu waling'oa na kupanda upya na sasa mazao yao yamestawi vizuri," anasema.

Kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa ya mwaka juzi yaliyochangia ukame ulionyausha mazao, Solomon anatoa mfano wa vijiji kama Kilimilile, Mabale na Nkerenge, vina kawaida ya kuathiriwa na ukame huo.

Anasema, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, ukame uliathiri mazao na maeneo hayo ambayo hayakuwa na njaa, badala yake kulikuwapo upungufu mdogo wa chakula na mavuno kwa baadhi ya wakulima.

Ofisa Kilimo huyo anasema maofisa ugani walishirikiana na viongozi wa vijiji na vitongoji, kusimamia mkakati wa wilaya kuzuia uuzaji wa mahindi mabichi, ili kuepukana na upungufu wa chakula katika eneo lao.

Pia, anasema waliwahimiza wananchi kujenga utamaduni wa kuhifadhi chakula, kabla ya kufanya mauzo na kuhamasisha ulimaji mazao yanayokomaa haraka na kustahimili ukame.

"Kwa kutumia vyanzo vya ndani



Mkulir hogo,

BIASHARA

**MTIHANI JINSIA MASOKO YA SHINYANGA**

Ukurasa 16

UCHUMI

**Yuko kidato nne, ameshawabunia wenzake mashine za pedi wajisitiri**

Ukurasa 18

BIASHARA

**Don Bosco yafungua mlango wa pili wa ofisi kupitia teknolojia**

Ukurasa 19

# asa

## apunguzwa

vya mapato na kwa kushirikiana na mradi unaohusiana na utunzaji mazingira, kujenga uwezo na kuwekeza katika shughuli za kilimo na mifugo katika wilaya zilizoko mipakani katika nchi za Tanzania, Uganda, Burundi na Rwanda (NSTP) yalisambazwa 'marando' ya viazi vitamu 534,000 na miche ya mihogo 388,400," anasema.

Solomon anasema, halmashauri hiyo ilitumia Sh.milioni tano kusambaza mbegu kwa wananchi na msisitizo wake ni hakuna msaada wa chakula uliopelekwa wilayani Misenyi, kukabili upungufu wa chakula.

Anasema tayari kuna mipango iliyowekwa kuhakikisha utunzaji mazingira na kusitokee uharibifu unaosababisha mabadiliko ya tabia nchi. Anahimiza umuhimu wa utunzaji chakula kinachotosheleza kaya, kuvusha msimu mmoja hadi mwingine. Anataja mazao yanayoweza kulimwa kwa wingi wilayani humo na kuhimili njaa ni; mahindi, mihogo, viazi vitamu, maharage, mtama na ulezi.


Kuhusu uwezo, halmashauri inazalisha chakula kwa tani 184,250. Hiyo inajumuisha ndizi, mahindi, maharage, mihogo, viazi vitamu na magimbi. Pia, Solomon anafafanua kuwapo uzalishaji mazao ya biashara tani 57,553 kila mwaka, ikijumuisha kahawa, miwa na vanilla.

**WANANCHI**

Abubakari Mohamed ni mkazi wa kijiji cha Kilimilile, anasema mwaka huo ukame uliathiri sana mazao yao na kuwa ni Mwenyezi Mungu tu ndiye aliyewanusuru.

"Suala la milo mitatu kwetu ilikuwa ndoto. Tulijitahidi kupata mlo mmoja ambao pia hatukushiba. Kama familia, ilikuwa na uwezo wa

**INATOKA UK.20**





Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kilimilile, katika Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, Iss- haka Yunusu, akifafanua jambo kuhusu kilimo chake. **PICHA ZOTE: LILIAN LUGAKIGIRA.**



ma Tadeo Bembwa (mwenye kofia kushoto), ambaye, alikuwa msambazaji mdogo rasmi wa mbegu za mi-
kutoka Kata ya Kasambya, akifafanua jambo kwa wageni wake shambani, mwaka 2016. **PICHA: MTANDAO.**

# Bosi Volkswagen kortini, 'akiteleza' jela miaka 10



Martin Winterkorn.

MAMBO bado sio shwari nchini Ujerumani kwa kampuni ya kutengeneza magari ya Volkswagen (VW) kuhusiana na sakata la kutengeneza magari yanayotoa moshi mwingi zaidi ya kiwango kinachoruhusiwa .

Wiki hii, Mtendaji Mkuu wa zamani wa kampuni hiyo, Martin Winterkorn (71), amepandishwa kizimbani akiwa na mabosi wengine wa zamani wanne, ambao hawakutajwa majina.

Pia, sakata hilo la magari kutoa moshi mwingi huko Marekani, VW inakabiliwa na shitaka hilo la moshi mwingi wa magari yake ya dizeli, lakini inaelezwa hakuna uwezekano wa Winterkorn kupelekwa huko.

Hiyo inatokana na Ujerumani kuwa na msimamo wa kutopeleka raia wake nje ya nchi kujibu mashitaka yanayowakabili. Mwendesha Mashitaka wa Ujerumani, alidai mahakamani kuwa Winterkorn, anakabiliwa na mashitaka ya kughushi, pia kukiuka sheria ya ushindani wa wazi.

Bosi huyo alijiuzulu wadhifa wake tangu Juni mwaka 2015, baada ya kukabiliwa na kashfa hiyo ambayo imechafua sana picha yake na kampuni, ikiendana na hasara kubwa iliyopatikana kwa Volkswagen.

Anadaiwa kwamba alipaswa kumfahamisha mmiliki wa kampuni na mamlaka za nchini Marekani, pia Umoja wa Ulaya, ambako magari hayo ya dizeli yameuzwa kwa wingi, lakini hakufanya hivyo. Pia, anatuhumiwa kuidhinisha kifaa 'feki; cha kuchuja moshi wa magari, ikawa mzizi uliozaa mapungufu mengi.

Inaelezwa kwa mujibu wa sheria anayoshitakiwa nayo, akitiwa hatiani kuna hatari ya kufungwa hadi kufikia miaka 10. Inaelezwa kifaa hicho feki, kiliwekwa katika jumla ya magari 600,000 ambayo yaliuzwa nchini Marekani mwaka 2009, pia nyinginezo nyingi katika maeneo tofauti duniani.

Kashfa hiyo iliibuliwa na watafiti kutoka Chuo Kikuu cha West Virginia, nchini Marekani mwaka 2009 na hapo utafiti kama huo ulisambaa katika maeneo mengine ya dunia yanayotumika magari, ikiwemo nchini Ujerumani.

Ni mkasa uliogharimu Volkswagen wastani wa Dola za Marekani bilioni 31 (Sh. trilioni 69.13) na Winterkorn, alishitakiwa rasmi mwezi uliopita.

Bosi wa sasa hivi aliyevaa kiatu hicho, Herbert Diess, anauponda uongozi wa mtangulizi wake, akisema anaamini katika kipindi hicho, kampuni ilikuwa taabani.

**BEI YA MAZAO >>** MCHELE 184375/- | ULEZI 142642.9/- **FEDHA >>** RAND 164.66 | KSH 22.75 | USH 0.61

BIASHARA

# MTIHANI JINSIA MASOKO YA SHINYANGA

• Amwagiwa matusi hadi akaacha biashara • Mamalishe halipwi kufikia mtaji 'unakata'
• Ustawi Jamii: Hatukujua...Agape waingilia • Sheria kali yaanza, 'vimini'navyo marufuku



Zuhura Athumani, muuza mboga katika soko la Ngokolo Mitumbani mjini Shinyanga Mjini, akisimulia yanayohusu ukatili wa kijinsia. **PICHA ZOTE: MARCO MADUHU**



Winifrida Mapunda, anayeuza mboga katika soko la Ngokolo Mitumbani mjini Shinyanga, akielezea yanayomsibu kazini.

**INATOKA UK.13**

Ni wastani wa miongo mwili tu iliyopita, ripoti za taasisi hizo za fedha, zilitawaliwa kwa njia ya maandishi, huku kiwango cha mawasiliano yake yakitawaliwa na mfumo wa analoingia, ikiwemo katika benki.

Lakini ghafla, mageuzi makubwa yanayofanyika duniani, sasa yameleta sura mpya katika mfumo wote wa fedha umezaa tija yenye sura nne kuu, ambazo ni: Usahihi, haraka, salama na huduma nyingi kama vile malipo kwa njia ya 'ATM' na mitandao ya simu.

Katika eneo hilo la mitandao ya simu ambayo inashika kasi zaidi, huduma za kuhifadhi, malipo na mikopo rahisi imezidi kutanuka, huku kukiwapo maendeleo makubwa ya ufanisi, hasa katika suala la malipo.

Ni moja ya maeneo yanayotiliwa mkazo, kupitia vyombo mbalimbali vya elimu na asasi za kiserikali, likiwemo jukwaa la ufundi nchini (Costech). Ikiwa ni mwendelezo wa elimu hiyo, Nipashe inayapata kutoka kwa watendaji wa kampuni ya simu ya Tigo, inaeleza hatua inayochukuliwa katika eneo la maboresho hayo ya kiteknolojia, ambazo kitaalamu zinaitwa 'Application' kazi zake ni nyingi zikiwemo usalama na ubora wake.

> **“Tumekuwa tukikidhi mahitaji ya matarajio ya wateja wetu, kwa namna ambayo wanataka mitandao yetu ya kijamii.**

Jerome Albou, Ofisa Mkuu wa Kitengo cha Ufundi, wa kampuni ya Tigo, anasema usalama kwa watumiaji wa huduma za kifedha kwa njia mpya ya simu anayoitambulisha kwa jina 'Tigo Pesa App,' kwamba inasaidia kuharakisha miamala ya kifedha, huku ikiwa rahisi kutumia.

Albou anasema, ni mfumo uliotengenezwa kwa namna rafiki na rahisi kila mtumiaji nchini. Anafafanua: “Tunasikiliza na kupokea maoni yanayotolewa na watumiaji na huwa tunachukua maoni pamoja na mapendekezo yanayotolewa na watumiaji 'App' hii na kuyaongezea kwenye mapitio ya kila mwezi.

“Tumekuwa tukikidhi mahitaji ya matarajio ya wateja wetu, kwa namna ambayo wanataka mitandao yetu ya kijamii,” anasema na kuongeza:

“ Pia, inatoa mchango mkubwa kuongeza uelewa kuhusiana na 'App' hii na kuwezesha kuiweka katika nafasi nzuri, huku tukiendeleza utamaduni wa kidigitali na kujenga ubunifu wa bidhaa zetu, kama ailivyo kawaida ya kampuni.”



Ofisa Miradi kutoka shirika la Agape mkoani Shinyanga, Mustapha Isabuda, akitoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanawake katika soko la Ngokolo Mitumbani, mjini Shinyanga.

### USALAMA JE?

Kuhusu usalama wa mfumo huo wa kiufundi, Albou anasema, imewekwa kiufundi, katika namna inayohakikisha taarifa zote za mtumiaji zinabaki salama, dhidi ya hujuma au kuingiliwa kwa namna yoyote, kupata taarifa hizo au kufanya muamala pasipo ruhusa ya mtumiaji.

Pia, anadokeza umuhimu wa mtumiaji kuhakikisha anaziweka taarifa zake salama, dhidi ya uwezekano wa kuingiliwa na mtumiaji mwingine, huku bosi huyo wa ufundi akitetea mfumo wake una kinga na usalama, wenye uhakikia wa ithibati ya kimataifa, inayotambulika kama 'GSMA' na 'ISO.'

“Kwa upande mwingine, pia tunafuatilia 'App' hii saa 24 kila siku ili kubaini majaribio yoyote ya hujuma au uhalifu kufanywa na tunapogundua uhalifu umefanyika, tunachukua hatua kwa kuongezea usalama zaidi,” anasema.

“Mbali na usalama eneo lingine analolitaja kuwa 'Tigo Pesa Apps' ni rafiki kwa mtumiaji ni kile anachokifatsiri ” inapatikana muda wote kwa njia tofauti” akitoa mifano mbalimbali.

Albou anaeleza nafasi ya mtumiaji wa kampuni yake ya simu, akitumia kauli: “Anapotaka kutuma pesa anaweza kutumia majina ambayo yapo kwenye simu yake, pasipo kulazimika kuandika namba pembeni.”

Anataja mustakbali huo, mbali na mtu mmoja mmoja, pia kuna njia za malipo ya simu na televisheni.

### INAPOKOSEWA JE?

Alipotakiwa na Nipashe kufafanua namna panapotokea makosa, Albou anasema, wanayarekebisha katika njia kuu mbili za malipo kurudisha fedha, wadau husika wanatumia njia mbili, moja ikiwa katika mfumo wa kawaida na nyingine katika mfumo wa malipo wa 'Tigo Pesa App'kwa kuzizuia zisitolewe na mtu aliyemtumia kwa makosa.

“Pesa zinaweza kurudishwa baada ya aliyetumiwa kukubali kuzirudisha kwa aliyemtumia kimakosa. Hata hivyo, ni muhimu kwa mteja kuhakikisha anakuwa makini anapotuma pesa kwa kuhakikisha namba anayotaka kuitumia pesa ni sahihi.

“Ili kumrahisishia mteja kutuma kwenye namba sahihi, tunamwonyesha jina la anayetaka kumtumia kabla ya kutuma. Endapo ataona jina ni sahihi, anaingiza namba yake ya siri, ikiisha anatuma,” anasema.

Anasema, huduma hiyo haifanyi kazi katika maeneo yasiyokuwa na mtandao wa intaneti kwa sababu za kiusalama, lakini ikitumika ambako kuna mtandao wa simu hiyo na hakuna 'kifurushi' husika, bado aina hiyo ya simu hizo ina njia mbadala iitwayo 'zero rated' akimaanisha haitozi gharama yoyote.

“Inaweza kufanya kazi kwenye mitandao mingine ya intaneti ikiwa ni pamoja na 'Wifi' lakini, kwa sababu za kiusalama, utahitajika kuweka neno la siri litalothibitisha kuwa wewe mtumiaji ndiyo mmiliki halali na ndiye anayetumia 'Tigo Pesa App' kufanya muamala,” anasema Albou

Huku akitumia tafsiri za kitaalamu, ofisa huyo wa ufundi, anahitimisha kuwa ni huduma zinazopatikana katika mifumo ya aina nyingi za simu ambazo zinaangukia huduma azozitaja za 'IOS.'

## Biashara katika picha



fisa Madini mkazi wa Mkoa wa Kimadini wa Simanjiro, Daudi Ntalima (kulia), akimuonyesha Waziri wa Madini, Dotto Biteko (watatu kushoto) eneo la machimbo ya madini ya Tanzanite Mji mdogo wa Mirerani alipotembelea jana. **PICHA: GIFT THADEY**



Mdau wa elimu na Mfanyabiashara, Erick Emmanuel (wa tano kushoto), akikabidhi mifuko 25 ya saruji kwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, kwaajili ya kusaidia kupunguza changamoto ya ukosefu wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari wilayani humo, mkoani Shinyanga jana. **PICHA: SHABAN NJIA**



Muuza pipi akiwa 'ameuchapa' usingizi wakati akisubiri wateja katika eneo la ukuta wa shule ya msingi Daimond, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MIRAJI MSALA**

**BEI YA MAZAO >>** MAHINDI 52625/-| MAHARAGE 170000/-

UCHUMI

TANZANIA YA VIWANDA SHULENI

# Yuko kidato nne, ameshawabunia wenzake mashine pedi wajisitiri

• Tathmini ya awali bei Sh. 200 • Ushuhuda ulimkera akaamua


**Na Augusta Njoji, aliyekuwa Bahi**

***WIKI mbili zilizopita, jarida hili lilikuwa na makala inayohusu changamoto ya wasichana masomoni, wanaokabiliwa na shida ya taulo za kike mkoani Dodoma na hatua zinazochukuliwa kujikimu kijamii kukabili changamoto hiyo. Katika mwendelezo huo, msichana wa Dodomna, amebuni mashine ya kutengeneza taulo za kike na kuingia katika kundi la wazalishaji. Kwa vipi? Fuatilia.***

LICHA ya serikali na wadau wa maendeleo kufungua milango zaidi kwa wasichana kupata elimu, bado wanakabiliwa na changamoto nyingi, ikiwamo upatikanaji wa taulo za kike kujisitiri.

Upande wa mabinti wa vijijini, ndiko kwenye hali mbaya zaidi kutokamna na umasikini wao. Wengi hulazimika kutohudhuria masomo katika siku hizo.

Sokoni bei ya paketi za taulo hizo zinafika kati ya Sh. 1,500 na Sh. 2,000





Mashine iliyobuniwa kutengeneza. Picha ndogo ni mbunifu wa pedi, Maleo Lameck (17). **PICHA ZOTE: AUGUSTA NJOJI.**

**UBUNIFU**

Katika sakata linaloendana na hilo, mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya sekondari Kondo, Maleo Lameck(17), Dodoma, amebuni mashine ya kutoa taulo za kike na kutoa mchango mkubwa wa kurahisisha upatikanaji wake.

Maleo anasema, amebuni mashine inayoitwa 'Pads Automatic Vending Machine' ambayo bidhaa yake itakapoingia sokoni, itauzwa kwa bei ya Sh.200 kila moja.

Mwanafunzi huyo mbunifu, anasema kiwango cha bei alichokipanga kinazingatia uwezo wa mwanafunzi.

"Ubunifu huu wa kutengeneza mashine ya kutoa taulo ulikuja pale tu mwenzangu alipoingia kwenye siku zake na akakosa pedi ya kujisitiri, akaamua kurudi nyumbani na kukosa masomo,"anaeleza.

Maleo anafafanua kuwa, ni jambo lilimsukuma azame katika uchunguzi kwenye shule mbalimbali kupata undani wa tatizo hilo na kubaini suluhisho la tatizo.

"Hili tatizo limesababisha idadi kubwa ya wanafunzi wa kike kuwa watoro na kufanya vibaya kwenye mitihani yao. Nimebuni hii mashine ambayo ikiwekwa kwenye chumba wanachotumia kujisitiri shuleni, mwanafunzi ataweka Shilingi 200 na atapata pedi ya kujisitiri na kurejea darasani kuendelea na masomo," anasema.

> **"Rafiki yangu alipokumbwa na hali hii, tulienda hadi kwa walimu kuomba lakini hakupata, akalazimika kurudi nyumbani na kukosa masomo.**

Anaeleza imani yake kwamba ubunifu huo utasaidia kupunguza tatizo, pindi wawapo shuleni na anafafanua: "Lengo la kutengeneza mashine hii ni iwekwe kama dharura shuleni ili kutoathiri masomo.

"Rafiki yangu alipokumbwa na hali hii, tulienda hadi kwa walimu kuomba lakini hakupata, akalazimika kurudi nyumbani na kukosa masomo."

Mwanafunzi huyo anasema, katika shule alizotembelea, mmoja wa walimu alimwambia katika kundi la wanafunzi 156 wanakosa masomo yao kila mwezi, wapo wengi wanakabiliwa na adha ya hedhi.

"Hawa wanafunzi ni wa darasa la nne hadi la saba, nilifikiria nibuni vifaa kama ATM hivi ndio nikabuni hii. Hii itasaidia sana, maana wengine wanaogopa au wanaona aibu kubeba pedi kwenye mabegi ya shule,"anasema na kuongeza:

"Nilichukua mwezi mzima kutengeneza hii mashine na nilipata mtu nikamueleza ninachotaka kutengeneza, akaniambia vifaa vinavyotakiwa, ili nitengeneze."

Maleo anasema katika mashine hiyo, zitanunuliwa pedi za kawaida na kuwekwa, mwanafunzi ataweza kuingiza Sh.200 na kupata pedi moja.

"Nafikiria pia kubuni mashine ambayo itatengeneza na kutoa pedi hapo hapo. Naamini, watu wenye viwanda wanaweza kuchukua ubunifu wangu na kutengeneza mashine nyingi zitakazonunuliwa na shule,"anasema.

**MAONO YAKE**

Wito wa Maleo kwa wanafunzi wa kike ni kutegemea makubwa kutoka kwake ili kuwawezesha mahudhurio ya uhakika masomoni.

Ombi la Maleo katika hilo, ni serikali kufanyia kazi ubunifu wake, ili kuwa na fursa itakayowawezesha watu kutoka mataifa mengine kujifunza kutengeneza mashine hizo.

"Pia wanafunzi ambao wana ubunifu wao na wamejificha wajionyeshe, ili serikali ikuze vipaji vyao kwa kuwa vitasaidia Tanzania yetu kufanikiwa katika uchumi wa viwanda,"anasema.

Juni mwaka jana, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango alitangaza kuondolewa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye taulo za kike nchini, ili kuweza kuwapa fursa wanafunzi waliopo shuleni na vijijini kuzipata kwa bei nafuu.

Anasema, serikali ilifanya uamuzi huo kutokana na sheria ya VAT kumpa mamlaka ya kufanya hivyo na anaongeza: "Napendekeza kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye taulo za kike.

"Lengo la hatua hii ni kuwezesha upatikanaji wa bidhaa hiyo adimu kwa bei nafuu ili kuweza kulinda afya ya mama na mtoto wa kike hasa watoto waliopo mashuleni na vijijini."

"Ni matarajio ya serikali, watengenezaji wa bidhaa wa taulo za kike watauziuza kwa bei nafuu baada ya kusamehewa kodi hii hatua," anafafanua.

**HATUA ZINGINEZO**

Mbali na hatua binafsi za uzalishaji na za kiserikali, kuna Mradi wa Usafi wa Mazingira (UMATA), unaotekelezwa na shirika la Plan International, wametoa mafunzo na kuwapatia vifaa wanafunzi wa shule ya msingi Mundemu wilayani Bahi, kwa ajili ya kutengeneza pedi kwa watoto wa kike.

Aidha, mwanafunzi wa darasa la saba Paulina Majengo, anaunga mkono kwamba hivi sasa wamepatiwa mafunzo ya kujihudumia wanapokuwa katika kipindi cha hedhi na wamejifunza namna ya kutengeneza pedi za asili, wanazotumia na wanafunzi wenzake.

"Zamani tulikuwa tunatoroka na kurudi nyumbani lakini hivi sasa yupo mwalimu ambaye anatusaidia kila tunapokuwa katika hedhi,"anasema Paulina.

Anasema, kutokana na uwepo wa chumba cha kujihifadhia kwa wanafunzi wa kike, ambacho kimejengwa maalum na kimekuwa msaada mkubwa kwao.

"Hivi sasa badala ya mwanafunzi kukimbilia nyumbani, anachokifanya hivi sasa ni kwenda katika chumba cha kujihifadhia ambacho kinakuwa na vifaa vyote, kama pedi pamoja na maji na baadaye anarudi darasani kuendelea na masomo kama kawaida," anasema.

FEDHA >> USD 2,300.96| Pauni 3,011.73| Euro 2,595.25

UCHUMI

# Don Bosco yafungua mlango wa pili wa ofisi kupitia teknolojia

- Waenda sambamba na Dira 2025
- Wajuzi wakutana waibuke upya

NA MARGARET MALISA



Wanafunzi wa Don Bosco wakiwa katika mafunzo mbalimbali. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

"NILIPOPATA nafasi ya kujiunga chuoni, ndoto yangu kubwa ilikuwa nitakapohitimu niende nikatafute ajira, niajiriwe, nifanye kazi kuendesha maisha yangu na wategemezi wangu.

"Nilipojiunga chuoni nilifundishwa umeme katika 'level' (hatua) ya kwanza, pili na tatu. Baadaye nikapata fursa ya mafunzo ya umeme wa sola. Hapo ndipo nilipobadili mawazo niliyokuwa nayo ya kusubiri kuajiriwa.

"Kwa sababu mafunzo niliyopewa, ninao uwezo wa kwenda kujiajiri mwenyewe na hata kutengeneza fursa kwa wenzangu, kupitia umeme mbadala wa sola," anasema Raymond Zabron.

Huyo ni miongoni mwa vijana waliopata fursa ya kupata mafunzo ya kufunga na kutengeneza umeme wa sola katika taasisi ya Don Bosco Net Tanzania na kuhitimu masomo yao hivi karibuni.

Akizungumza na Nipashe hivi karibuni, Mussa anasema matumizi ya umeme wa sola ni fursa itakayopanua ajira kwa wengi, hivyo itasaidia kuokoa maisha ya wengi vijijini.

"Kwa hiyo, japo nilitamani nikaajiriwe kwenye mashirika makubwa, sasa nimebadili mtazamo wangu kabisa. Nikitoka hapa nakwenda kujiajiri, sitasubiri tena kuajiriwa, kwa sababu umeme wa sola naona una fursa kubwa ya kutengeneza ajira.

"Pia, tutaweza kusaidia jamii ambayo bado inaishi gizani. Wapo Watanzania hasa kule vijijini bado wanatumia mishumaa, vibatari, nyenzo ambazo ni changamoto, kwani wakati mwingine huwa hatari kwao, nyumba huungua moto.

"Baadhi ya vituo vya afya havina umeme. Kule vijijini, watu wanapata shida kwa kutumia njia hii mbadala ya umeme wa sola, tutasaidia kuwaokoa," anasema.

**UHALISIA SOKONI**

Katika mkutano wa wadau 57 wa nishati mbadala ulioandaliwa na taasisi ya Don Bosco Tanzania na kuwakutanisha vijana waliopata mafunzo katika vyuo hivyo na wadau hao

Meneja Miradi wa Taasisi ya Don Bosco Network Tanzania, Rosemary Terry, anasema upo umuhimu mkubwa kusaidia vijana kupata ujuzi mbadala, hasa wakati huu wa mwelekeo wa Tanzania na Uchumi wa Kati, ifikapo mwaka 2025.

"Kwa sababu vijana wakipatiwa ujuzi mbadala utawawezesha kujiajiri na si kusubiri kuajiriwa wanapokwenda katika soko la ajira. Hii ni mbinu itakayosaidia kukabili changamoto ya ukosefu wa ajira nchini.

Anasema nishati mbadala ni sekta mojawapo ambayo ikifanyiwa kazi kwa kuhakikisha vijana wanapata ujuzi unaohitajika sokoni, wanaweza kuajiriwa au kujiajiri wenyewe.

> **Baadhi ya vituo vya afya havina umeme. Kule vijijini, watu wanapata shida kwa kutumia njia hii mbadala ya umeme wa sola, tutasaidia kuwaokoa.**

"Hivyo, Don Bosco tumeanza kujikita katika suala hili, leo (jana) tumeona vyema tukutane na wadau hawa ili kujadiliana nao kuweza kupata maoni yao jinsi tunavyoweza kuboresha ufundishaji wetu," anasema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Rex Energy, Francis Kibisa, anasema wazo hilo ni zuri, kwani kampuni zilikuwa zinapata vijana ambao hawana ujuzi wa kutosha unaohitajika katika soko la ajira.

Anasema vijana wengi wanaotoka katika elimu za juu hupatiwa mafunzo ya kufanya kazi za ofisini.

"Lakini, kiuhalisia vijana walioko kwenye vyuo vya ufundi, ndiyo wanaokuwa na ujuzi muhimu unaohitajika hasa kwa shughuli za nishati mbadala, ambazo uhitaji wake upo zaidi maeneo ya vijijini.

"Kwa hiyo, hili linatusaidia sisi waajiri, tumeona upo umuhimu wa kushirikiana na Don Bosco kwa kuwapa nafasi ya mafunzo ya muda mfupi ili vijana wanaokuwa wamepata mafunzo waje kwenye kampuni yetu kufanya kazi, kwa njia hii tutaweza kujua yupi anafaa na kwa aina ipi ya kazi," anasema.

**MRATIBU DON BOSCO**

Mratibu wa Shughuli za Ajira Don Bosco, Oswald Manyerere, anasema kazi yake kubwa ni kuwaunganisha vijana wanaomaliza masomo na ulingo wa ajira.

"Tunahakikisha tumewaandaa kwenda 'kupambana' katika ulimwengu wa ajira, tunajua haitoshi kijana kuwa na ufundi pekee, lazima awe na mambo mengine yanayomsaidia kuwa bora zaidi.



"Tunawafundisha maadili binafsi, maadili ya kazi na kuwapa ujuzi wa kujiajiri au kuajiriwa katika kampuni mbalimbali na tumefanikiwa kwa kushirikiana na kampuni mbalimbali," anasema.

Tangu kuanzishwa nchini miaka ya 80, Taasisi ya Don Bosco Net Tanzania, jukumu lake ni malezi, makuzi na mafunzo stadi za maisha kwa vijana wa kike na kiume wanaotoka katika mazingira magumu.

Tayari kuna maelfu ya vijana walionufaika na ujuzi walioupata kutoka taasisi hiyo kwa kujiajiri au kuajiriwa katika ofisi na viwanda mbalimbali nchini.


# Takwimu za Biashara

Na Edward Ntwale & Elias Samweli

Bei ya Mazao Ya Chakula kwa Sh/kilo 100 Aprili 18, 2019

| Mkoa | Arusha | D'Salaam | Dodoma | Geita | Morogoro | Kagera | Kilimanjaro | Kigoma | Lindi | Manyara |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 57000 | 70000 | 53000 | 57000 | 48000 | 60000 | 40000 | 45000 | 80000 | 60000 |
| Mchele | 200000 | 210000 | 195000 | 130000 | 165000 | 185000 | 180000 | 160000 | 200000 | 200000 |
| Mtama | 40000 | 60000 | 35000 | 180000 | 71000 | 100000 | 80000 | 100000 | 150000 | 42000 |
| Uwele | 40000 | 60000 | 34000 | 180000 | 71000 | 110000 | NA | 100000 | NA | 100000 |
| Ulezi | 72000 | 140000 | 75000 | NA | 155000 | 150000 | 180000 | 150000 | 200000 | 120000 |
| Ngano | 87000 | 130000 | 160000 | 180000 | 163000 | NA | 98000 | 150000 | NA | 120000 |
| Maharage | 150000 | 220000 | 170000 | 170000 | 185000 | 150000 | 180000 | 140000 | 200000 | 130000 |
| Viazi Mviringo | 70000 | 80000 | 66000 | 70000 | 82000 | 75000 | 50000 | 90000 | 100000 | 60000 |

## Mwenendo wa Shilingi




## Mafuta

Bei : Kuanzia Machi 6, 2019

| MKOA | DSM | Arusha | Pwani | Dodoma | Geita | Iringa | Kagera (Bukoba) | Katavi | Kigoma | Moshi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Petroli | 2,098 | 2,191 | 2,102 | 2,157 | 2,263 | 2,162 | 2,313 | 2,306 | 2,329 | 2,181 |
| Dizeli | 2,131 | 2,195 | 2,135 | 2,189 | 2,296 | 2,195 | 2,346 | 2,339 | 2,362 | 2,185 |
| M'Taa | 2,096 | 2,286 | 2,101 | 2,155 | 2,262 | 2,161 | 2,312 | 2,304 | 2,328 | 2,276 |

## Soko la Hisa la Dar es Salaam Kikao cha Aprili 18, 2019

### Muhtasari

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 3,256.85 | -68.53 |
| DSEI | 1,980.73 | -45.71 |
| Thamani za Hisa (bln) | 19,091.95 | |
| Mauzo | 229,689,375.00 | |
| Hisa | 659,575 | |

### Zilizopanda na Zilizoshuka

| Kampuni | Bei | Badiliko |
|---|---|---|
| ACA | 5,150 | -8.04% |
| NMB | 1,980 | -15.38% |
| EABL | 4,760 | -2.46% |
| NMG | 1,500 | +7.14% |

### Viwango vya kubadilisha

| Fedha | Nunua | Uza |
|---|---|---|
| EUR | 2,578.38 | 2,605.09 |
| USD | 2,278.12 | 2,300.91 |
| KES | 22.57 | 22.75 |
| GBP | 2,986.62 | 3,017.64 |

## Bei za hisa hadi kikao cha Aprili 17, 2019

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| CRDB | 125.00 | 125.00 | 0 |
| ACA | 5,150 | 5,600.00 | -8.04 |
| DCB | 340 | 340 | 0 |
| DSE | 1,260 | 1,260 | 0 |
| EABL | 4,760.00 | 4,880.00 | -2.46 |
| JHL | 9,150.00 | 9,150.00 | 0 |
| KA | 120.00 | 120.00 | 0 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| KCB | 1,020.00 | 1,020.00 | 0 |
| MBP | 490.00 | 490.00 | 0 |
| MCB | 500.00 | 500.00 | 0 |
| MKCB | 800.00 | 800.00 | 0 |
| MUCOB | 400.00 | 400.00 | 0 |
| NICO | 170.00 | 170.00 | 0 |
| NMB | 1,980.00 | 2,340.00 | -15.38 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| NMG | 1,500.00 | 1,400.00 | 7.14 |
| PAL | 400.00 | 400.00 | 0 |
| SWALA | 490.00 | 490.00 | 0 |
| SWIS | 1,700.00 | 1,700.00 | 0 |
| TBL | 10,000.00 | 10,000.00 | 0 |
| TCC | 17,000 | 17,000.00 | 0 |
| TCCL | 600.00 | 600.00 | 0 |

## VIWANGO VYA KUBADILISHA FEDHA

| FEDHA | KUNUNUA | KUUZA |
|---|---|---|
| KENYA SHS | 2,253.37 | 2,271.41 |
| UGANDA SHS | 57.41 | 61.52 |
| RWANDAN FRANC | 251.53 | 254.55 |
| BURUNDI FRANC | 218.12 | 219.77 |
| USD | 227,815.84 | 230,094.00 |
| POUND STG | 297,322.45 | 300,410.73 |
| EURO | 257,454.68 | 260,121.27 |
| CANADIAN $ | 170,802.10 | 172,458.40 |
| SWITZ. FRANC | 225,806.17 | 227,973.84 |
| JAPANESE YEN | 2,034.43 | 2,054.23 |
| SWEDISH KRONOR | 24,671.95 | 24,907.88 |
| NORWEG. KRONOR | 26,898.06 | 27,151.02 |
| DANISH KRONOR | 34,494.56 | 34,838.97 |
| AUSTRALIAN $ | 163,822.37 | 165,506.61 |
| INDIAN RPS | 3,282.18 | 3,313.95 |
| PAKISTAN RPS | 1,531.45 | 1,620.38 |
| ZAMBIAN KWACHA | 18,373.74 | 18,668.88 |
| MALAWIAN KWACHA | 289.30 | 308.71 |
| MOZAMBIQUE-MET | 3,537.51 | 3,567.35 |
| ZIMBABWE $ | 42.63 | 43.49 |
| SDR | 316,657.19 | 319,823.76 |
| GOLD (T/O) | 290,625,352.56 | 293,599,230.71 |
| S. AFRICAN RAND | 16,293.16 | 16,444.33 |
| UAE DIRHAM | 62,031.22 | 62,634.47 |
| SINGAPORE $ | 168,440.55 | 170,099.80 |
| HONK KONG $ | 29,040.36 | 29,330.02 |
| SAUD ARABIAN RIAL | 60,747.65 | 61,353.49 |
| KUWAIT DINAR | 749,369.57 | 756,589.50 |
| BOTSWANA PULA | 21,460.25 | 21,858.93 |
| CHINESE YUAN | 34,061.34 | 34,394.75 |
| MALAYSIA RINGGIT | 55,121.18 | 55,632.01 |
| SOUTH KOREA WON | 201.06 | 203.05 |
| NEWZEALAND | 153,320.06 | 154,899.28 |

## Interbank Foreign Exchange Market (IFEM)

| Tarehe | Idadi (Mn USD) | Juu | Chini | Wastani |
|---|---|---|---|---|
| **17/Apr/2019** | **2.20** | **2,308.00** | **2,298.45** | **2,300.94** |
| 16/Apr/2019 | 2.10 | 2,308.00 | 2,298.40 | 2,300.84 |
| 15/Apr/2019 | 1.70 | 2,316.00 | 2,298.40 | 2,300.93 |
| 11/Apr/2019 | 1.50 | 2,309.00 | 2,298.45 | 2,300.94 |

## Inter-bank Local Money Markets

| Tarehe | Kiasi (million-TZS) | Juu | Chini | Wastani (WAR) |
|---|---|---|---|---|
| **17/Apr/2019** | **41,200** | **5.50** | **5.00** | **5.29** |
| 16/Apr/2019 | 53,550 | 5.50 | 4.90 | 5.24 |
| 15/Apr/2019 | 18,450 | 6.00 | 5.25 | 5.44 |
| 11/Apr/2019 | 39,000 | 6.00 | 5.00 | 5.15 |
| 10/Apr/2019 | 43,300 | 6.00 | 4.90 | 5.18 |
| 9/Apr/2019 | 40,100 | 5.50 | 4.90 | 5.04 |

# Hali ya hewa ilivyotoa darasa kukabili mtikisiko uchumi

kutumia kilo mbili za unga(kwa siku), ililazimika kutumia kilo moja na kunywa maji mengi kujaza tumbo," anasema.

Anasema upungufu huo wa chakula ulisababisha hata afya za watoto, hasa wenye umri wa chini ya miaka mitano, kuyumba na wengine kupungua uzito, akitoa mfano wa mwanawe aliyekuwa na miaka miwili, alipungua uzito kutoka kilo tisa hadi 8.7.

"Nilishtushwa, pamoja na uhaba mkubwa wa chakula tuliokuwa nao, niliamua bora wengine tushindie maji, lakini mtoto huyo tuhakikishe anapata chakula ili kuokoa afya yake iliyokuwa inaelekea hatarini," anasema.

Anasema yeye na wanakijiji wenzake waliokuwa na mifugo kama mbuzi na ng'ombe, walilazimika kuuza mifugo kwenda kuhemea chakula, huku wasio nayo waliishia kwenda kuomba kazi za vibarua, ili wapatiwe mbadala wa chakula.

Mohamed anasema kuwa mvua zilipoanza kunyesha walipanda mazao yanayokomaa katika kipindi kifupi, vikiwamo viazi vitamu, ndipo baada ya miezi mitatu walianza kuvuna na kupunguza makali ya njaa.

"Mimi na familia yangu tulifikia hatua ya kula maembe na mafenesi. Tulinunua unga kama nusu kilo, tukakoroga uji, harafu tukakata maembe na mafenesi na kuyatumia kama vitafunwa na baada ya hapo tulikunywa maji mengi," anasema.

Anasema katika msimu wa kilimo ulioanza Septemba mwaka jana, kulijitokeza dalili za ukame kujirudia, kwani mvua zilichelewa na kusababisha baadhi ya maeneo mazao kama mahindi na maharage kuathirika.

"Baadhi yetu mvua zilipokosa hatukupanda, tulisubiri mvua, lakini hata walipanda yalikauka na kulazimika kuyang'oa na kupanda upya. Sasa yanaonyesha matumaini na mvua zimeanza kunyesha, tuna imani tutaweza kuvuna," anasema.

Mohamed anakumbula tabu nyingine walioipata ni kusumbuliwa na magonjwa ya mazao yanayoshambulia viazi na mihogo, huku akikumbuka kwa kufanana kuhusu wanawe kwamba: "Walilia sana kusababisha mama yao kulia."

**MWENYEKITI KIJIJI**

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kilimilile, Iss-haka Yunusu, anasema wakati wa ukame, mbali na mazao kukauka, pia mifugo kama ng'ombe na mbuzi ilikufa kwa kukosa malisho.

**MENEJA HALI YA HEWA**

Steven Malundo ni Meneja wa Mamlaka ya Hali ya Hewa mkoani Kagera, anayesema mvua za vuli kwa mkoa wa Kagera huwahi ni ikianza mwezi Septemba.

Malundo anasema, katika utabiri wao wa awali wa msimu wa vuli, walieleza kuwa mkoani humo mvua zitakuwa za wastani hadi chini ya wastani.

Anawataka wakulima kuwasiliana na maafisa ugani ili kupanga kulima kulingana na msimu ulivyo, na kuwa wakulima waambiwe mazao ya kupanda kulingana na hali ya hewa ilivyo.



## HABARI MBEYA

# Polisi yajipanga kulinda amani Pasaka

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limesema limejipanga kikamilifu kuimarisha ulinzi kwenye viunga vyote vya mkoa huo ili kuhakikisha wakazi wote wakiwamo wageni wanasherehekea Sikukuu ya Pasaka kwa amani na utulivu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei kwa vyombo vya habari, historia inaonyesha katika vipindi vya sikukuu matukio mbalimbali ya uhalifu yamekuwa yakitokea na kwamba Jeshi la Polisi limejipanga kudhibiti matukio hayo.

Matei alisema kwa sababu Mkoa wa Mbeya unapakana na nchi jirani ya Malawi pia barabara kuu ya Tanzam, Jeshi linafanya doria na misako ya mara kwa mara ili kuhakikisha usalama kwa watumiaji wa barabara wakiwamo madereva na watembea kwa miguu.

"Kuelekea Sikukuu za Pasaka, Jeshi la Polisi linatoa wito kwa watumiaji wote wa barabara kuzingatia sheria, alama na michoro ya usalama barabarani ili kuepuka ajali zinazoweza kuepukika sambamba na hilo, tumejipanga vizuri kuhakikisha maeneo yanayohatarisha usalama wa raia kama vile Mlima Nyoka, Mlima Iwambi, Mlima Igawilo na Mwansekwa, ulinzi na usalama umeimarishwa," alisema Matei.

Aidha, aliwasisitiza waumini wa madhehebu ya Kikristo katika Sikukuu ya Pasaka kushiriki katika ibada/misa kwa nyakati tofauti kulingana na ratiba zao kutosita kutoa taarifa mara wanapoabaini hali ya uvunjifu wa amani, lakini alisema Jeshi la Polisi limejipanga kuhakikisha ulinzi na usalama katika makanisa hasa katika misa au ibada za mkesha.

Alitoa wito kwa viongozi katika makanisa kuhakikisha wanaweka utaratibu mzuri hasa katika suala la ulinzi kwa kuzitumia kamati za ulinzi na usalama ili kuhakikisha katika maeneo ya ndani na nje ya makanisa hasa sehemu za maegesho ya magari pana kuwa salama.

Vilevile alisisitiza kwa wamiliki wa kumbi za starehe kufuata sheria hasa kuzingatia leseni zao za biashara zinavyowaelekeza ikiwa ni pamoja na kuzingatia muda wa kufungua na kufunga sehemu zao za biashara, wenye kumbi za muziki kuhakikisha kumbi zao zinaingiza idadi ya watu inayohitajika pamoja na kuweka walinzi katika maeneo yanayowazunguka.

"Tunasisitiza wazazi pamoja na walezi kuwa makini na watoto katika Sikukuu ya Pasaka na kwamba wanapaswa kuongeza uangalizi kwa watoto wao kila mahali wanapokwenda iwe makanisani, misikitini au katika maeneo yenye michezo ya watoto," alisema Matei.




Naibu Waziri wa Kilimo, Omar Mgumba (wanne kulia) ambaye alikuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa maabara ya Shule ya OCP Kijiji cha Isansa, Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali wa mkoa huo, akiwamo Mkurugenzi wa OCP, Dk. Mshindo Msolla (wanne kushoto) na wageni waalikwa katika uzinduzi huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 12.8/- kukarabati barabara Mbeya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 12.8 kwa ajili ya kujenga na kukarabati miuondombinu ya barabara na madaraja kwa kiwango cha lami na changarawe katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya ikiwa ni Mpango wa Mradi wa Uendelezaji Miji kimkakati yaani TSCP.

Hayo yalisemwa jana na Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura), Mhandisi Alberto Kindole, akiwa na Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Mbeya mjini ambayo ilifanya ziara ya kukagua miradi ya barabara ambayo inatekelezwa na Tarura. Kindole alisema fedha hizo ambazo zimetolewa na serikali zitasaidia kujenga miundombinu ya barabara zenye urefu wa kilometa 6.78 katika Jiji la Mbeya.

Alizitaja barabara hizo kuwa ni ya Viwandani hadi Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (Must), Iyela na Mwakibete na kwamba barabara zote hizo zitakamilika mwezi Septemba, mwaka huu.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbeya Mjini, Afrey Msomba, alisema ameridhishiwa na utekelezaji wa miradi hiyo na kutaka wanaopotosha kwenye mitandao ya kijamii kuwa serikali hajifanya jambo kwenye ujenzi wa miundombinu wachukuliwe hatua.

Msombe alisema baadhi ya wananchi sio wazalendo kazi yao ni kupinga na kutoa lugha za kejeli katika kila jambo la maendeleo linalofanywa na serikali na kwamba hawatavulimia vitendo hivyo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alisema ofisi yake kwa kushirikiana na wataalam wataendelea kusimamia kwa karibu ujenzi huo na kwamba thamani ya fedha iliyotolewa itaendana na miundombinu itakayoajengwa.

Baadhi ya wananachi akiwamo Salim Mtete, walisema kukamilika kwa barabara hizo kutaondoa changamoto za usafiri hasa nyakati za masika na kuwaomba wakandarasi kukamilisha kwa wakati.

# H'shauri Mbarali yamaliza mgogoro

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, imesema imemaliza mgogoro uliodumu kwa muda mrefu kati ya wafugaji wa vijiji 10 na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, ambao ulisababishwa na tozo ya Sh. 100,000 kwa kila mfugo unaoingia hifadhini.

Mgogoro huo ulimalizwa jana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo ikiongozwa na Mwenyekiti wake ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, wakati wa ziara ya kukagua maeneo mbalimbali ya wafugaji na Hifadhi ya Ruaha.

Aidha Katika ziara hiyo wafugaji wa vijiji 10 ambavyo ni Magigiwe, Iwalanji, Mapogoro, Igunda Magwali, Luhanga na Iyala Vikae, Ikanutwa na Mwanamvalawalimweleza Mkuu wa Wilaya kuwa wamekuwa wakitozwa faini ya shilingi laki moja kwa kila Ng'ombe kwenye maeneo ambayo sio ya Hifadhi.


Kutokana na maelezo hayo Mfune aliagiza kusitisha mgogoro huo na kuzitaka pande zote mbili kutumia busara ili kuepusha malalamiko na kusisitiza kila mmoja kutimiza majukumu yake bila kuvunja sheria.

"Naomba mgogoro huu usitishwe, wafugaji wasitozwe tena faini wala mifugo yao kukamatwa, uongozi wa hifadhi ya Ruaha muendelee kutoa elimu kwa wakulima na wafugaji bila kukoma ili kila mmoja afahamu mipaka yake, wakati serikali ikiendelea na mchakato wa upatikanaji wa suluhu ya kudumu ambao upo katika hatua za mwisho za umaliziwaji wake," alisema Mfune.

Mfune alisema uamuzi wa kusitiza mgogoro huo utasaidia viongozi wa Kata, Vijiji na Hifadhi kukaa meza moja kuonyesha maeneo ya msingi ambayo yalikwishalipwa fidia na ambayo bado hayajalipwa ili wafugaji waweze kujua wanaishia wapi wanapokwenda kulisha mifugo yao wakati wakisubiri maelekezo ya mwisho ya mpaka wa kudumu kutoka Serikali Kuu.

Alisema Halmashauri tayari ilieleza maeneo yote ya mpaka, na ambayo watu walishalipwa kwamba hairuhusiwi kuingiza mifugo, kwa wale watakaotaka kukiuka utaratibu huo watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Kiongozi wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Agricola Lihiru, alimshukuru Mkuu wa Wilaya kwa kutatua changamoto hiyo na kueleza kuwa wafugaji wengi walikuwa wanahisi wanaonewa pindi inapokamatwa mifugo ndani ya Hifadhi ya Ruaha. Aliwaomba wafugaji kuheshimu mipaka ya hifadhi kwa kutoingiza mifugo na kwamba yapo maeneo ambayo yalitengwa kwa ajili ya shughuli za ufugaji.





# Wanne wanaswa kwa utapeli kujifanya maofisa wa serikali

**Na Elisante John,** SINGIDA

WATU wanne wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Singida kwa tuhuma mbalimbali ikiwamo utapeli na kujifanya watumishi wa umma katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida, kutoka kitengo cha mapato.

Akizungumza na Nipashe katika kituo kikuu cha polisi jana, Kamanda wa Polisi mkoani Singida, Swetbert Njewike, aliwataja watu hao kuwa ni Frank Biseko (30), Hashimu Hassan (27), Ramadhan Shaban (36) na Said Athumani (40), kutoka Mtaa wa Sokoine, Minga, Kanarakana na Majengo.

Alisema kuwa, watuhumiwa hao kwa pamoja walijifanya watumishi kutoka kitengo cha mapato na kujipatia zaidi ya Sh. 800,000, kutoka kwa vijana walioahidiwa kupata kazi ya udereva wa magari na kukusanya ushuru kwenye maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Singida.

Kamanda Njewike alisema kuwa, baada ya polisi kupata taarifa za wahalifu hao, vijana wake walifanya upelelezi uliofanikisha kuwatia mbaroni watuhumiwa hao wakati wakiwa kwenye pilikapilika za kutekeleza zaidi njama zao.

Aidha, Njewike alisema kuwa katika kudhibiti hali ya usalama ndani ya mji wa Singida, jeshi hilo lilifanikiwa kukamata vitu mbalimbali ikiwamo kompyuta mpakato, ving'amuzi vya runinga, redio ndogo, nguo na viatu, mali ambazo zimeibwa kutoka kwa rai wema.

Alifafanua kuwa watuhumiwa wote wanatarajiwa kufikishwa mahakamani wakati wowote baada ya upelelezi kukamilika ili wakajibu tuhuma zao zinazowakabili. Katika hatua nyingine Kamanda Njewike alisema, kipindi cha kuelekea sikukuu ya Pasaka, jeshi hilo limejiimarisha zaidi kila kona ya mkoa ili kudhibiti njama zozote za uhalifu, ikiwamo wizi, matumizi ya dawa za kulevya na matumizi mabaya ya barabara ili kudhibiti ajali.

Alisema pia jeshi hilo linawakumbusha wazazi na walezi kutunza usalama wa watoto wadogo na vijana wao wanaotoka majumbani kwenda kusherehekea sikukuu ya Pasaka, kwa kuhakikisha wanarejea salama nyumbani badala ya kunogewa na sherehe kwenye kumbi za starehe.

"Kipindi hiki cha kuelekea sikukuu ya Pasaka, ninawaomba wakazi wa mkoa wa Singida, watii sheria bila shuruti, lakini wale wachache wanaotarajia kuvunja sheria kwa makusudi, basi wajue wazi Jeshi la Polisi litawadhibiti na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria," alisema.

Kamanda Njewike aliwapongeza wananchi wa mkoa huo wanaoendelea kuwa watiifu kwa mamlaka husika ikiwamo dola, hali iliyowezesha mkoa kuwa shwari, na hivyo kulipunguzia mzigo Jeshi la Polisi katika kukabiliana na uhalifu.



Mwenyekiti wa Bodi ya Nne ya Uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali nchini, Dk. Faustine Sambaiga (kushoto), akizungumza na wajumbe, wakati wa kikao cha 40 cha bodi hiyo, kilichofanyika jijini Dodoma jana. Kulia ni Kaimu Msajili wa mashirika hayo, Neema Mwanga. **PICHA: WAMJW**

## Serikali 'yafyekelea mbali' NGO 7

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BODI mpya ya kusimamia mashirika yasiyo ya kiserikali imeyafuta mashirika matano kutokana na kukiuka mila na tamaduni za nchi pamoja na miongozo iliyowekwa na serikali.

Akizungumza na waandishi wa habari Kaimu Mkurugenzi wa bodi hiyo, Neema Mwanga, aliyataja mashirika hayo kuwa ni CHESA Community Health, Education Service & Advocacy, KBH Sisters, AHA Development Opportunity, Path Finder, Green City & Others na Hamasa Radiation.

Alifafanua kuwa mashirika hayo yamekuwa yakifanya ufadhili wa misaada kinyume cha sheria na taratibu za nchi.

Aliyataka mashirika mengine yajifunze kutoka kwa wenzao ambao wamefutiwa usajili kwa kuendesha mambo ambayo hayaruhusiwi na sheria za nchi.

Alisema kwa mamlaka waliokuwa nayo hawatakuwa tayari kuangalia upuuzi unaofanywa na mashirika hayo ukizingatia yanakwenda kinyume na sheria za nchi.

Aliyataka mashirika yote nchini kufuata mila na desturi za nchi ambazo zimewekwa kwa mujibu wa sheria.

Naye Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Richard Sambaiga, alisema sheria inayohusu mashirika yasiyo ya kiserikali ni lazima ifuatwe.

"Kwa kuwa inabidi tuwe wajali kama bodi kwa sababu tunaona wanakiuka sheria," alisema Dk. Sambaiga.

Alisema hakuna kitu kigeni kinachotakiwa zaidi ya kufuata sheria za nchi ili kazi zifanyike kwa ufasaha kama serikali inavyoagiza.

Aliongeza kuwa lengo la bodi hiyo siyo kukomoana kama ambavyo wanavyohisi wadau wa mashirika hayo.

# Vijana, wanawake wakacha mikopo ya halmashauri

**Na Elisante John,** SINGIDA

KASI ya vijana, wanawake na walemavu kukopa fedha zilizotengwa na serikali katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida, imeelezwa kuwa ya kiwango cha asilimia 50 pekee, hali inayozorotesha jitihada za makundi hayo maalumu kuweza kujikomboa kiuchumi.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya Singida, Veronica Mure, alisema hayo juzi kwenye mafunzo ya kada mbalimbali wakiwamo vijana, chini ya Shirika la Maendeleo na Elimu (MEDO), Lenye lengo la kuitaka jamii kulipa kodi ili kujiletea maendeleo yao. Alifafanua kuwa ingawa ni muhimu kwa makundi hayo kuimarika kiuchumi ili kuvunja vikwazo walivyonavyo, lakini bajeti ya zaidi ya Sh. milioni 64 zilizotengwa na serikali mwaka wa fedha unaoisha Juni mwaka huu ni Sh. milioni 31 pekee ndizo zimekopwa na vijana.

Alisema kuwa kwa uhalisia unavyoonyesha ni wazi vijana bado wanakabiliwa na tatizo katika kujiunga kwa njia ya vikundi vya uzalishaji mali, ili waweze kunufaika na fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya ustawi wa maisha yao.


"Baadhi ya vikundi ambavyo tayari vimenufaika na mikopo iliyotolewa, vingine miradi yao siyo ya tija hali inayosababisha baadaye kusambaratika na hivyo marejesho inakuwa shida," alisema Mure.

Kutokana na hali hiyo, ofisa maendeleo ya jamii wa halmashauri hiyo, alitoa wito kwa vijana kuanzisha miradi na kusajili vikundi vyao kabla ya kuomba mkopo, ili waweze kujipatia maendeleo ya kiuchumi kupitia fedha ziazotolewa na serikali.

"Vijana wengi hawatumii fursa hiyo, lakini wanabakia kulalamika...tatizo ni nini vijana? Kwa kweli mnanipa shida sana ya kufikiri niwafanyie nini mpaka munielewe vyema kwa ajili ya kujitokeza mkope fedha zenu," alisisitiza Mure.

Kwa upande wake Joachim Muyawani wa Asasi ya BLUWAT inayojihusisha na utafiti, kupitia Shirika la Actionaid, kwa ufadhili wa Shirika la Ushirikiano na Maendeleo la Norway(NORAD), aliwataka wananchi kulipa kodi serikalini ili wanufaike na huduma bora za kijamii.

Alisema iwapo jamii wakiwamo vijana watashiriki ipasavyo katika shughuli za uzalishaji mali, watajihakikishia kipato cha uhakika, na hivyo sehemu ya faida watalipa kodi serikalini, ambayo itatumika kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwamo elimu, afya, barabara na maji.








Meneja wa Tigo Kanda ya Kusini Mashariki, Abbas Abdulrahman (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya shilingi milioni moja kwa wakala wa huduma ya Tigo Pesa, Shine Murtazah wa mkoa wa Iringa juzi, ambaye ni mmoja kati washindi wawili wa kanda hiyo, waliojishindia zawadi za fedha taslimu kwenye promosheni ya 'Cash In' iliyomalizika mwishoni mwa mwezi Machi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri haridhishwi vita dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Yussuf Masauni, amesema haridhishwi na kasi ya mapambano ya dawa za kulevya Visiwani Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Zanzibar, alisema kutokana na kutoridhishwa na hali hiyo amemtaka Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo kuunda timu maalum itakayofanya kazi ili kuwabaini askari polisi ambao wamekuwa wakishiriki katika kuzorotesha mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Alieleza upo upungufu kwa baadhi ya askari wa Jeshi la Polisi kutokana na kuwapo kwa tuhuma za baadhi ya askari wa jeshi hilo kuharibu kesi za dawa za kulevya kwa makusudi.

"Pia kuna tuhuma kwa baadhi ya askari wa Jeshi la Polisi Zanzibar wanachukuwa rushwa kwa wauzaji wa dawa za kulevya ambao wanajulikana, lakini wanaendelea kutanua mitaani," alisema Naibu Waziri huyo.

Alisema hawezi kuona hali hiyo ikiendelea kwa kuwa vijana ambao ndio nguvu kazi ya taifa wanaharibika na kuwa kama mazezeta ambao vijana hao walitakiwa kujenga taifa lao.

Aidha, alisema kuwa uchumi wa nchi unaathirika, maadili ya jamii yanaharibika kwa sababu ya watu waliopewa dhamana kushindwa kutekeleza majukumu yao katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Hata hivyo, Masauni alieleza masikitiko yake makubwa kutokana na kutopata ushirikiano kutoka kwa Katibu wa Tume ya Kupambana na Dawa za Kulevya katika kupata vielelezo na taarifa za ziada ili kukamilisha majukumu yake. Alieleza katika tume hiyo alitaka vielelezo na taarifa hizo dhidi ya tuhuma zilizotolewa kwa Jeshi la Polisi kuhusu kuzorotesha kwa kesi za dawa za kulevya ili askari waliohusika kuweza kuchukuliwa hatua za kisheria.

"Hatuwezi kuathiri askari ambao wanafanya kazi nzuri kwa wazembe wachache na wapuuzi waliomo ndani ya jeshi hili," alisema Naibu Waziri huyo.

Masauni alisema anayo baadhi ya majina ya askari polisi wanaodhorotesha kesi za dawa za kulevya na uchunguzi utakapokamilika wahusika wote watachukuliwa hatua za kisheria.

# ZEC yaita wanafunzi kujiandikisha

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) imewataka wanafunzi ambao wamefikisha umri wa miaka 18 kuhakikisha wanajiandikisha katika daftari la mpigakura zoezi hilo litakapoanza kwa waandikishaji wapya.

Hayo yameelezwa na Ofisa Uchaguzi wa Wilaya ya Magharibi A Unguja, Suluhu Ali Rashid, wakati akitoa elimu juu ya umuhimu wa kupiga kura kwa wanafunzi wa kidato cha nne wa Shule ya Sekondari Bumbwini Makoba Wilaya ya Kaskazini "A" Unguja.

Alisema wanafunzi ambao waliomaliza kidato cha nne na wale waliopo shuleni na wameshafikisha umri wa miaka 18 wanapaswa kujiandikisha katika kuelekea uchaguzi wa mwaka 2020.

Alisema hatua ya kutoa elimu kwa wanafunzi shuleni imefikiwa baada ya kufanya utafiti mdogo na kubaini vijana wengi ambao wanatimiza umri wa miaka 18 hawana mwamko wa kushiriki katika uandikishaji wa wapigakura, hali inayowafanya kupoteza haki yao ya msingi katika kuchagua viongozi watakao waletea maendeleo.

Aidha, alisema kuwategemea wazazi peke yao kuwahamasisha watoto wao juu ya kushiriki uchaguzi inaonekana ni changamoto kwa baadhi ya vijana, hivyo wameona ni vyema kuanza elimu hiyo ambayo itasaidia vijana kuwa na mwamko wa kushiriki.

Alieleza wanafunzi wanapaswa kwanza kuhakikisha wanapata vitambulisho vya Uzanzibari ukaazi vitakavyowawezesha kufanikisha zoezi la uandikishaji kwa kuwa ambae hana kitambulisho hicho atakuwa hana sifa katika uandikishaji wa wapigakura utakapoanza.

"Wanafunzi wanapaswa kwanza kuhakikisha wanavitambulisho vya Mzanzibari mkazi na tumeona wanafunzi wingi wa sekondari hawana vitambulisho, hivyo kutokana na ndio kwanza wamefikisha umri wa miaka 18 mwaka huu, tunawahamasisha kuwa navyo mapema ili zoezi la uandikishaji likianza na wao wajiandikishe," alisema.

Aliwataka wanafunzi hao wakaanze utaratibu wa kupata vitambulisho vya ukaazi mapema pamoja na kuwa mabalozi kwa wanafunzi wenzao kwa kuwahamasisha katika ushiriki wa zoezi hilo muhimu kwa maendeleo yao kwa kuwapata viongozi chaguo lao.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzake, Khamis Yusuph, aliwaomba maofisa hao wa tume kuwasaidia katika zoezi hilo kwa sababu lina ugumu hususan katika kupata barua kutoka kwa mashekha.

# Kiwanda cha mafuta kujengwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SHIRIKA la kimataifa linalojishughulisha na uzalishaji wa kilimo cha alizeti la Alemdar kutoka Uturuki limeonyesha nia ya kutaka kujenga kiwanda kitakachozalisha bidhaa kwa kutumia malighafi ya maua.

Lengo limeelezwa kuwa ni kuitikia wito wa serikali wa kuwa nchi ya viwanda katika kipindi kifupi kijacho.

Ofisa Mkuu wa Shirika hilo, Fatma Atala, alieleza hayo wakati ujumbe wa viongozi wa shirika hilo ulioongozwa na Mwenyekiti wake, Oktay Alemder, ulipokutana kwa mazungumzo na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, Vuga Mjini Zanzibar.

Fatma alisema mradi huo wa kibiashara endapo utafanikiwa kuanzishwa Visiwani Zanzibar unalenga pia kuwashirikisha wakulima vijijini kwa kulima maua ya alizeti katika baadhi ya maeneo yao ya kilimo.

Alisema maua ya alizeti ni bidhaa inayoendelea kuwa na hadhi kubwa katika masoko ya kimataifa ambayo inaweza kusaidia kunyanyua mapato ya washiriki katika ukulima wake sambamba na kuongeza pato la taifa.

Naye Balozi Iddi, aliueleza ujumbe huo wa viongozi wa shirika hilo kutoka Uturuki kwamba Tanzania tayari imeshaamua kuwa nchi ya viwanda ifikapo mwaka 2025.

Balozi Iddi alisema wawekezaji wa ndani na nje ya nchi wana fursa ya kuitumia nafasi hiyo katika ushiriki wao wa uwekezaji utakaokwenda sambamba na azma hiyo ya serikali.

Hata hivyo, alieleza kwamba ujumbe huo unapaswa kuzingatia zaidi mazingira halisi ya Zanzibar yanayoendelea kukumbwa na changamoto ya ufinyu wa ardhi.

Balozi Iddi aliushauri ujumbe huo kutayarisha maombi na kuyawasilisha kwa Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) kwa hatua ya kuangalia uwezekano wa kuufanyia uchambuzi yakinifu mradi wao na mazingira halisi ya ardhi yaliyopo Zanzibar. Aidha, aliuhakikishia ujumbe huo kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko tayari muda wowote kuunga mkono jitihada za shirika hilo za kutaka kuitumia fursa ya uwekezaji.

## Akamatwa kanisani akiwa na Petroli, kibiriti

**Washington,** MAREKANI

JESHI la Polisi nchini Marekani, limesema linamshikilia mwanamume mmoja ambaye aliingia kwenye Kanisa la Mtakatifu Patrick jijini New York, Marekani, akiwa amebeba makopo mawili ya Petroli, kibiriti.

Walinzi walimkabili mtu huyo mwenye miaka 37 alipokua akiingia katika kanisa hilo siku ya Jumatano jioni. Taarifa kutoka Jeshi la Polisi limeeleza kuwa mtu huyo alimwaga mafuta chini ndipo maafisa wa polisi wakamkamata kumpeleka mahabusu.

Naibu Kamishna wa Polisi, John Miller alisema tukio hilo linaloshukiwa kuwa baya lilitokea siku mbili baada ya kanisa la Notre-Dame jijini Paris kuungua moto.

"Mtu alikua akitembea usawa wa kanisa amebeba magaloni ya mafuta, na vibiriti, ni jambo la kushukiwa," alisema Miller.

Afisa wa intelijensia na masuala ya ugaidi alisema ni mapema sana kueleza kama kusudio la mtu huyo ni kutekeleza vitendo vya kigaidi

Taarifa zaidi zilieleza kuwa alipokabiliwa nje ya Kanisa, mwanamume huyo aliwaambia maafisa kuwa gari yake iliishiwa mafuta na alikua akipita mbele ya kanisa hilo ili kulifikia. **BBC**

## Tshisekedi kuzuru eneo la ajali

**KINSHASA,** Congo

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Felix Tshisekedi, anatarajiwa kuzuru eneo la ajali ya boti iliotokea Aprili 15 katika Ziwa Kivu.

Katika ajali hiyo watu 25 wanadaiwa kupoteza maisha huku watu wengine zaidi ya 150 hawajulikani walipo. Juhudi za kuwatafuta manusura kutokana na ajali hiyo zinaendelea.

Taarifa rasmi zinaeleza kuwa watu 25 wamepoteza maisha, huku matumaini ya kuwapata watu wakiwa hai yakitoweka.

Katika Wilaya ya Kelehe ambako kumetokea ajali hiyo, hakuna timu maalumu ya uokozi, ambapo wavuvi wa eneo hilo ndio waliojitokeza na kutoa msaada wa kuwaokoa na kukusanya miili ya watu waliopoteza maisha. Kaimu Mkuu wa Wilaya hiyo, Oli Bizimungu alielekea katika eneo la tukio na kufanya sensa ya watu kwa kupita kijiji kwa kijiji, ambapo alibaini watu 96 hawakuwapo katika makazi yao na hawajulikani walipo.

Kwa kawaida uwezo wa mitumbwi hiyo ni kubeba watu wasiozidi 50 pamoja na mizigo.

Hata hivyo, kwa mujibu wa viongozi wa bandari ya Goma, watu wasiozidi 40 ndio waliorodheshwa kusafiri na boti hiyo, lakini huenda njiani walichukuwa watu wengine ambapo mashahidi wanasema boti hiyo ilikuwa imepakia idadi kubwa ya abiria.

Wakati Rais Thisekedi akitarajiwa kuzuru eneo hilo, viongozi wa kijeshi wamekwenda kukutana na manusura. Rais Tshisekedi ameahidi kuanzisha uchunguzi na wahusika wataadhibiwa kwa mujibu wa sheria. **RFI**

# Rais Salva Kiir 'ajitosa' kupatanisha mzozo Sudan

**JUBA,** Sudan Kusini

RAIS wa Sudan Kusini, Salva Kiir, amejitolea kuwa mpatanishi katika kuidhinisha mageuzi ya kisiasa nchini Sudan, baada ya kupinduliwa kwa kiongozi aliyekuwapo Rais Omar al-Bashir.

Hatua hiyo imekuja ikiwa imepita miezi saba baada ya Bashir kusaidia katika upatanishi na kufikiwa makubaliano ya amani kati ya Rais Kiir na kundi kuu la waasi wa upinzani Sudan kusini.

"Rais amejitolea kuwa mpatanishi katika majadiliano ya makundi tofauti nchini Sudan kwa matumaini kwamba mageuzi mapya yataidhinisha siku mpya Sudan," ilieleza taarifa kutoka ofisi ya rais Sudan Kusini.

**Takribani watu 400,000 wameuawa na karibu theluthi ya idadi ya wananchi wa taifa hilo imeachwa bila ya makazi.**

Inafahamika kwamba Bashir alikuwa na jukumu kubwa katika kuhakikisha makubaliano ya amani Sudan Kusini yanafikiwa.

Mataifa hayo mawili yana historia ndefu na huenda ndio sababu Sudan Kusini inaona ina wajibu wa kuhusika katika yanayoshuhudiwa hivi sasa Sudan.

Sudan kusini ilijitenga na Sudan mwaka 2011 na miaka miwili baadaye taifa hilo changa lilitumbukia katika vita vya kiraia.

Takribani watu 400,000 wameuawa na karibu theluthi ya idadi ya wananchi wa taifa hilo imeachwa bila ya makazi.

Rais Salva Kiir na aliyekuwa makamu wake Riek Machar wametia saini makubaliano ya amani hivi karibuni kumaliza mzozo huo wa miaka mitano.

Ni makubaliano yaliofikiwa kwa usaidizi wa Sudan, lakini Riek Machar alisema hayuko tayari kurudi Juba na anataka mipango ya kuunda serikali ya muungano iahirishwe mpaka masuala ya usalama yatakapo tatuliwa nchini.**BBC**



Mojawapo ya wapiganaji nchini Libya wakiwa katika mapigano. **PICHA: ALLIANCE**

# Ujerumani yafanya kikao kuhusu Libya

**BERLIN,** Ujeruman

SERIKALI ya Ujerumani jana iliitisha mkutano wa dharura wa Baraza la Umoja wa Usalama kujadili hatua za kuchukuliwa katika vita vinayoendelea Libya.

Hatua hiyo imekuja baada ya bodi ya watu15 kushindwa kufikia muafaka wa makubaliano ya pamoja ya kuweka chini silaha Libya.

Tangu kuzuka kwa mapigano Libya wiki mbili zilizopita, watu 205 wameuawa huku 900 wakijeruhiwa katika mapambano yanayoendelea karibu na mji Tripoli.

Jana bodi hiyo ilitofautiana namna ya kuushughulikia mzozo wa Libya baina ya jeshi la Libya (LNA) na serikali ya makubaliano ya kitaifa iliyoko Tripoli, (GNA).

Mjumbe wa Umoja wa Mataifa nchini Tripoli, Ghassan Salame alitaka mapigano hayo yasitishwe mara moja kwa usalama wa raia milioni tatu.

Kauli yake imejiri saa chache baada ya mizinga ya mabomu kufyatuliwa usiku katika kijiji kimoja kilichoko katika wilaya ya Abu Salimu kusini mwa Tripoli.

Waziri wa Usalama wa Ndani wa Serikali ya Tripoli, Fathi Bashagha, anamshutumu Khalifa Haftar kwa mauaji yanayoendelea.

"Huu ni uhalifu wa kivita na huyu Khalifa Haftar hana akili ni Field Marshal. Huwezi kuamini kwamba anaweza kuua watu wake namna hii. Kulipua mizinga Tripoli na unajua kuna watu wengi hapa, zaidi ya milioni tatu. Huyu ana wazimu ni zaidi ya Adolf Hitler," alisema Fathi.

Wananchi nchini Libya wanasema wamevunjwa moyo na jumuiya ya kimataifa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwa sababu waliwatarajia watachukua hatua madhubuti kuwasimamisha wauaji na uovu unaoendelea.

Ujerumani ambayo kwa sasa ndio kiongozi wa Baraza la Usalama itatoa mapendekezo yake baada ya kusikiliza taarifa mbali mbali kuhusiana na hali inavyoendelea nchini Libya.

Haftar amekuwa akiungwa mkono na nchi za Misri, Umoja wa nchi za Kiarabu na Saudia, Urusi na Ufaransa. **DW**

# Waandishi wa habari wawili wahukumiwa miaka 30 jela

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WAANDISHI wa habari Christopher Gamaina wa gazeti la Raia Mwema na Zaphania Mandia wa Channel 10, wamehukumiwa kwenda jela miaka 30 na Mahakama ya Wilaya Magu, mkoani Mwanza.

Pamoja na waandishi hao, watu wengine wawili wamehukumiwa miaka minne jela kila mmoja.

Waandishi hao walishtakiwa kwa kosa la unyang'anyi wa kutumia nguvu Desemba 27, mwaka 2017 majira ya saa nane mchana katika eneo la Isandula, wilayani Magu.

Walidaiwa kutumia nguvu kumnyang'anya Pastory Nkwabi na Tizira Enock na kujipatia Sh. 3,000,000.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Wakili wa washtakiwa hao, Linus Amri, alidai wateja wake walifunguliwa kesi ya jinai namba 11 ya 2018 katika Mahakama ya Wilaya ya Magu, mkoani Mwanza na kusikilizwa na hakimu Kente na Mwendesha Mashtaka Chacha.

"Wateja wangu ambao wamehukumiwa ni Christopher Gamaina mwenye umri wa miaka 44, Zephania Mandia (38), Manga Msalaba (39) na Wilfred Robert (38), wote wakazi wa Mwanza," alidai Linus.

Naye Mwenyekiti wa waandishi wa habari wa kupiga vita matumizi ya dawa za kulevya na uhalifu (OJADACT) na anayejihusisha na Mtandao wa watetezi wa haki za binadamu THRDC, Edwin Soko alisema, wameazimia kukata rufaa.

"Mimi kama mwenyekiti wa waandishi wa habari wa kupiga vita matumizi ya dawa za kilevya na uhalifu OJADACT na pia mwanaharakati wa uhuru wa habari nasema tumeazimia kukata rufaa ili kesi hii isikilizwe hivyo tunawaomba waandishi wote watulie wakili wetu wa watuhumiwa ameanza taratibu za kuandika rufaa Jumanne baada ya sikukuu ya Pasaka," alisema Soko.

Aidha soko alisema: "Kimsingi hukumu hii sio mwisho wa kutafuta haki kwa waandishi wenzetu, kwa kuwa walikumbwa na mkasa huo wakiwa kwenye majukumu yao ya kutafuta habari."



Vijana wakifanya kibarua cha kusafisha miwa kwa ajili ya kukamua juisi, katika eneo la Msimbazi, jijini Dar es Salaam jana. Miwa 20 husafishwa kwa gharama ya 1,500/-. **PICHA: MIRAJI MSALA**

MTIKISIKO

# Wenyeviti 13 wajiuzulu wahamia CCM

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WENYEVITI 13 wa vitongoji katika Jimbo la Hai, mkoani Kilimanjaro ambalo linaongozwa na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Freeman Mbowe (Chadema), wameitikisa tena ngome ya chama hicho, baada ya kujiuzulu nyadhifa zao na kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Kundi hilo la wenyeviti hao wa vitongoji, linaivuruga ngome hiyo, huku ikiwa imepita miezi saba tangu Wenyeviti wa Serikali za Vijiji 19 katika halmashauri ya wilaya hiyo ambao wanatoka Chadema, kubwaga manyanga na kujiunga na CCM, Septemba 6, mwaka jana.

Mbunge wa Jimbo la Hai ni Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Mbowe.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kupokea barua za kujiuzulu kwa wenyeviti hao, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Yohana Sintoo, alithibitisha kupokea barua za kujiuzulu kwa wenyeviti hao 13 jana asubuhi.

"Leo Aprili 18 (jana), nimepokea barua za kujiuzulu wenyeviti 13 wa vitongoji kwa tiketi ya Chadema na mchakato rasmi wa kujaza nafasi hizo tutatizama wakati tukielekea kwenye mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika mwezi Oktoba mwaka huu," alieleza.

Aliwataja wenyeviti waliojiuzulu na vitongoji vyao kwenye mabano kuwa ni Gladson Swai (Bomani), Ruyandumi Kimaro (Makiweru-Uswaa), Beda Msofe (Lembeni B-Rundugai), Ndemael Massawe (Nure-Ng'uni), Leonard Urassa (Njoro Chini-Shirinjoro) na Raymond Mushi (Nkwelengy-Nronga).

Wengine ni Filbert Usiri (Nkwamandaa-Nronga), Eliatosha Lema (Maaseni-Nronga), Majisia Paul (Ngulujuu-Chemka), Nimkaza Mhando (Kikuletwa-Chemka), Gasper Mwasha (Boma Kati-Kware), Walter Swai (Masamu-Uswaa) na Majinsi Nyange (Lembeni A-Rundugai).

Muda mfupi baada ya wenyeviti hao kubwaga manyanga, walikwenda hadi Ofisi za CCM, Wilaya ya Hai na kupokelewa na wajumbe wa kamati ya siasa wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa wilaya hiyo, Wang'uba Magai.

Baada ya tukio hilo, Katibu wa CCM wa wilaya hiyo, Kumotola Kumotola, aliwaeleza wenyeviti hao na wajumbe wa kamati ya siasa kwamba uamuzi huo mgumu waliochukua wenyeviti wa vitongoji ni zawadi tosha ya Sikukuu ya Pasaka ya kumpa Mwenyekiti wa CCM Taifa na Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli.

"Hii ni zawadi tosha ya kumpa Mwenyekiti wetu wa taifa wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli. Kwa uamuzi huu wa wawakilishi wa wananchi wa Hai, ni vizuri Freeman Mbowe (Mbunge) akajitathmini na kuona kuna haja ya kujiuzulu na kuwapa nafasi wananchi wengine wa Hai kuongoza," alieleza Kumotola.

# Kortini tuhuma kuingiza kifaa cha mawasiliano

**Na Hellen Mwango**

WATU wawili na kampuni moja, akiwamo raia wa Kenya, Brian Lusiola na Meneja Uendeshaji wa Biashara wa Kampuni ya Inventure Mob Tanzania Ltd, Ahmed Ngassa, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wakikabiliwa na mashtaka sita ikiwamo kuingiza kifaa cha mawasiliano bila kibali cha Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na kuisababishia serikali hasara ya Sh. milioni 64.2.

Mbali na Lusiola na Ngassa, mtuhumiwa mwingine ni Kampuni ya Inventure Mobile Tanzania Ltd., inayofanya biashara na Tala Tanzania.

Washtakiwa wote walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Wakili wa Serikali, Jackline Nyantori, alidai washtakiwa wakiwa katika jengo la Tanzanite Park, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, walitenda makosa hayo, huku wakijua ni kinyume cha sheria.

Alidai katika shtaka la kwanza, katika tarehe isiyofahamika kati ya Januari Mosi na Desemba 31, 2018, wakiwa katika jengo hilo washtakiwa waliingiza kifaa cha mawasiliano kinyume na sheria chenye jina la Proliant MLI GEN 9 Server (PABX Virtual Machine yenye serial number 76520D88838129_425) bila kuwa na kibali kutoka TCRA.

Katika shtaka la pili, washtakiwa hao pamoja na kampuni hiyo, kinyume na sheria wanatuhumiwa kati ya tarehe hizo na katika jengo hilo, walisimika kifaa hicho na kuendesha mtambo huo wa mawasiliano bila kuwa na kibali kutoka TCRA.

Alidai katika shtaka la tatu washtakiwa hao pamoja na kampuni hiyo wanatuhumiwa kutoka Januari 2 hadi Machi 11, 2019, waliendesha kifaa hicho cha kielektroniki cha mawasiliano kwa kuruhusu simu za kimataifa zilizoingia nchini bila kibali cha TCRA.

Katika shtaka la nne, washtakiwa hao pamoja na kampuni hiyo wanatuhumiwa kutoka Januari 2 hadi Machi 11, 2019 kumiliki kifaa hicho kilaghai, wakiwa na nia ya kukwepa gharama za uendeshaji kwa ajili ya kupokea na kusambaza mawasiliano, walisambaza simu hizo za kimataifa nchini. Katika shtaka la tano washtakiwa hao wanatuhumiwa kutumia kifaa hicho kilichounganishwa na mawasiliano kwa nia ya kupokea na kusambaza mawasiliano bila kupata kibali.

Nyantori alidai katika shtaka la sita, kwa matendo yao ya makusudi waliisababishia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na TCRA hasara ya Sh. 64,260,000.

Hakimu Shaidi alisema washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka ya uhujumu uchumi na mahakama yake haina mamlaka ya kuisikiliza.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GRACE BINGILEKI MATONDANE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T. 510 AYE.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DAR/OST/RB/397/2019.**

115188602

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**NANZOKE THEOBALD MVUNGI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 141 DPT TOYOTA IST.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **KW/BJ/WL.201.**

115188302

RAISSA COMPANY LIMITED

## MNADA WA HADHARA

Kwa Idhini tuliyopewa na AML FINANCE LTD,tutauza kwa mnda wa hadhara gari ya mdaiwa T156 AAD LANDCRUISER PRADO gari ipo katika yard yetu ya Makumbusho.Lengo nikufidia/kupunguza deni la mkopo analodaiwa.Mnada utafanyika tarehe 20/4/2019 saa 3 asubuhi mahali dhamana ilipo.Mteja atalipa 25% baada ya mnada, 75% ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi na mnada utarudiwa, Gharama zakubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Kwa mawasiliano tupigie namba hapo juu au fika ofisi za AML finance Lufungira.**

115188502

JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
18/04/2019

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAPILI tarehe 21/04/2019 kampuni ya **TARIMO REMI STANSLAUS** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **MACHAME GATE** kuelekea **ENGARUKA na kutoka ENGARUKA** kuelekea ARUSHA, gari hilo lenye namba za usajili: **T155BJM/T916DCG.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 17.50**
   **Upana – mita 3.28**
   **Kimo – mita 4.60**
3. Njia itakayotumika **MACHAME GATE hadi ENGARUKA** kuptia **MAKUYUNI na kurudi ARUSHA** kupitia , **MAKUYUNI** gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115187402

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 81/2019**

**Ombi la HALIMA HAMAD KAZIMOTO Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HAMAD JOJI KAZIMOTO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/04/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 18/04/2019.

115188102

## TANGAZO LA KAZI

Shirika la **HEALTH PROMOTION TANZANIA (HDT)** Linatangaza nafasi ya kazi , Meneja wa program ufuatiliaji wa sera na ushawishi (Program Manager Policy Monitoring and Advocacy)

Sifa na wajibu wa muombaji (ToR) vinapatikana kwenye Tovuti ya shirika **www.hdt.or.tz.**

Maombi yafanyike kwa kujaza fomu ya maombi inayopatikana kwenye tovuti ya Shirika **www.hdt.or.**

Maombi haya yatumwe kwetu kupitia barua pepe **info@hdt.or.tz.**

**Mwisho wa kuomba maombi haya ya kazi ni Ijumaa 3 Mei 2019.**

115186402

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu:+255 26 2324455
Fax: +255 26 232233
Barua Pepe ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
18/04/2019.

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAMOSI tarehe 20/04/2019 kampuni ya **M.E & CO. LTD** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa Kutoka LINDI kuelekea MOROGORO ,
   Gari hilo lenye namba za usajili:

   **T802 AJN HORSE/ T812 AKE TRAILER**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu -mita 22.00
   Upana -mita 3.50
   Kimo -mita 4.80
3. Njia itakayotumika **LINDI** hadi MOROGORO kupitia **DAR ES SALAAM.** gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115187302

## KUPOTELEWA NA KADI ZA MAGARI

**NICOSTA ACADEMY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili

**T 581 DNB NISSAN CARAVAN.**

**T 309 DEA TOYOTA NOAH.**

Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **KW/RB/211/19.**

115187202

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI.

**ESTINO SEVELIN MSANZI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za Usajili T. 256 AHE aina ya TOYOTA COASTER yenye chasis Na. **JTGFB518801003988** Na Ingine Na. **1HZ0389577.**

Kwa atakayeiona atoe Taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu nae.

**Taarifa ya Polisi: IR/RB/1482/2019.**

115188502


NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga Simu: 0767 223 311

*KWA MATANGAZO MADOGO, MADOGO*

*Tupigie 0767 223311*

## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# GIROUD ADOKEZA ATAKATAA MKATABA MPYA




**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI, Olivier Giroud amedokeza kwamba anaweza kukataa ofa ya kuongeza mkataba mpya hapo Stamford Bridge.

Giroud tayari anakaribia mwishoni mwa mkataba wake wa miezi 18 aliosaini wa pauni milioni 18 wakati alipohama kutoka Arsenal na kutua hapo Chelsea Januari mwaka jana.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwenye umri wa miaka 32 amefunga mabao tisa kwenye Kombe la Europa msimu huu, na kumfanya kuwa mfungaji bora wa michuano hiyo.

Lakini ufungaji wake kwenye Ligi Kuu England ni hafifu kwani amefunga mabao mawili tu baada ya kuanza katika mechi saba kati ya mechi 24 alizoichezea.

Chelsea bado ina nafasi ya kuongeza mkataba kwa miezi 12 hadi mwishoni mwa msimu huu, na anaweza kuondoka akiwa mchezaji huru.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Daily Mirror, hakuna mazungumzo yoyote yaliyofanyika hadi sasa na hivyo inamuacha Giroud na sitofahamu juu ya majaliwa yake ya baadae.

"Sifurahii kuwa chaguo la pili. Kitu cha muhimu kwangu ni kupata dakika za kutosha kucheza. Mimi ni mshindani, hivyo nataka kupata nafasi zaidi ya kucheza," amesema akinukuliwa na Daily Mail.

# Barca wana matumaini kumtwaa de Ligt

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona imebakiwa kuwa na matumaini kuwa, nahodha wa Ajax, Matthijs de Ligt, atajiunga nao katika kipindi cha majira ya joto, licha ya chipukizi huyo kuchelewa kutangaza majaliwa yake ya baadae.

De Ligt amekuwa akihusishwa na mpango wa kutua pale Camp Nou kwa muda mrefu, huku pia akihusishwa na mpango wa kutakiwa Juventus, ambayo ilitolewa katika hatua ya robo fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya na sasa pia Manchester United.

Barca waliweza kumshawishi Frenkie de Jong kuthibitisha hatima yake mapema Januari kwa euro milioni 86 ambapo atajiunga nao kipindi cha majira ya joto.

Kwa mujibu wa Daily Mail, miamba hao wa Katalunya wamefanya kila kitu kinachohitajika kwa ajili ya kumfanya nyota huyo mwenye umri wa miaka 19, De Ligt kujiunga nao msimu ujao.

Makubaliano yanasemwa yameanza na wana imani kubwa kuwa nyota huyo atajiunga nao kipindi cha majira ya joto.

Daily Mail linatambua kwamba De Ligt anasubiria kuona itakapofikia Ajax kwenye ligi ya mabingwa Ulaya.

Hivyo ni kwamba, wana imani kubwa nyota huyo atamfuata patina wake de Jong kujiunga na Barcelona.






# Conte akaribia kutua Juventus

**ROME,** Italia

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Antonio Conte alifanya mazungumzo ya awali kwa ajili ya kurudi Juventus mwishoni mwa msimu huu.

Conte mwenye umri wa miaka 49 amekuwa hana kazi tangu Julai mwaka jana wakati Maurizio Sarri alipochukuliwa kwenda Stamford Bridge kuchukua nafasi yake, wiki chache baada ya kufukuzwa klabuni hapo.

Lakini Conte anaweza kurudi kwenye familia aliyoizoea msimu ujao wakati Sky Sports ikiripoti kwamba mabingwa hao wa Serie A, Juventus wamefanya mazungumzo na Mtaliano huyo juu ya uwezekano wa kupewa nafasi hiyo.

Bianconeri hao walitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katika hatua ya robo fainali Jumanne iliyopita na Ajax.

Juve wamekuwa miamba watatu wa Ulaya kukumbana na kasi ya vijana hao wa Uholanzi baada ya Bayern Munich kutoka nao sare mara mbili kwenye hatua ya makundi, huku Real Madrid wakitolewa hatua ya 16 bora.

Na baada ya kumaliza 'njaa' yao ya kusubiri ubingwa wa ligi hiyo ya Ulaya kwa kipindi cha miaka 23, huku majaliwa ya Massimiliano Allegri yakionekana kuwa kwenye wakati mgumu.

Allegri ametumia miaka mitano iliyopita mjini Turin, ikishinda mataji mfululizo na amebakiwa na mwaka mmoja kwenye mkataba wake wa sasa na Juventus.

# SON HEUNG-MIN ALIKUWA HAJUI KAMA ATAIKOSA AJAX




**MANCHESTER,** England

TOTTENHAM Hotspurs itakuwa bila ya mshambuliaji wake, Son Heung-min katika mchezo wa kwanza wa hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Ajax.

Son amefungiwa mechi ya kwanza itakayopigwa jijini London baada ya kuonyeshwa kadi ya tatu ya njano kwenye michuano hiyo wakati walipofungwa magoli 4-3 na Manchester City juzi Jumatano.

Raia huyo wa Korea Kusini alifunga mara mbili kuiwezesha Spurs kufuzu kwa mabao mengi ya ugenini, akiwa pia alifunga bao la ushindi kwenye mchezo wa kwanza wakati wakiibuka na ushindi wa goli 1-0 siku nane zilizopita.

Lakini Tottenham hawataweza kumchezesha katika mchezo huo wakati Ajax watakapowafuata kwenye uwanja wao mpya, baada ya Son aliyeonyeshwa kadi ya njano kwa kumvuta shati, Kevin De Bruyne baada ya kipindi cha pili.

Heung-Min Son alijulishwa kufungiwa mchezo mmoja wakati akihojiwa na televisheni ya Ujerumani kuhusu kuukosa mchezo huo wa kwanza wa nusu fainali.

Son hakuwa anajua kwamba ataukosa mchezo wa kwanza hadi pale alipoulizwa na mtangazaji wa televisheni hiyo ya Ujerumani, kwani anajisikiaje.

Na yeye akajibu: "Sijui."

# *Rashford 'agomea' mkataba mpya*

**MANCHESTER,** England


MARCUS Rashford bado hajafikia makubaliano juu ya mkataba mpya na Manchester United, huku mshambuliaji huyo akiendelea kuhusishwa na uhamisho wa kwenda Barcelona kipindi cha majira ya joto.

Tetesi hizo zilikuwa zinasambaa wakati United ikielekea kwenye mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya miamba wa Katalunya Jumanne, wakati wakipigwa mabao 3-0.

Na sasa inaonyesha kuwa Rashford bado hajakubali kusaini mkataba mpya na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 anataka kuongezewa mshahara hadi pauni 200,000 kwa wiki, huku mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2020. Habari zaidi zinasema kwamba kocha, Ole Gunnar Solskjaer ana nia ya kumbakisha mchezaji huyo, lakini ni wazi kwamba itategemea na makubaliano yao wenyewe.

"Ole anataka kumbakisha kikosini mwake na ana mipango naye ya muda mrefu, lakini yeye bado hajafikia mwafaka," limeandika gazeti la Daily Mail.

Haya hivyo, taarifa zaidi zinasema kuwa, yeye mwenyewe ana ndoto788 ya kutaka kwenda kucheza kule Barcelona, ingawa miamba hao wa Katalunya bado hawajaonyesha nia hiyo.




# Guardiola alia na VAR

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola ameonekana kutofurahishwa na uamuzi uliofanywa kupitia 'VAR' ambao umepelekea kupewa goli mpinzani wao Tottenham, huku kwa upande wao wakinyimwa bao la dakika za mwisho lililofungwa na Raheem Sterling.

Kupitia mahojiano yake na waandishi wa habari mara baada ya kumalizika kwa mechi hiyo, Guardiola amesema kuwa anaunga mkono mfumo huo mpya, lakini katika upande mmoja na kwa upande mwingine bao la Fernando Llorente mkono ndiyo umeufuata mpira na siyo mpira umeufuata mkono.

"Na kubaliana na VAR, lakini pengine kwa upande mwingine Fernando Llorente mkono uliufuata mpira (aliunawa), huwenda kwa upande aliyokuwapo mwamuzi haukuonyesha hivyo," amesema Guardiola.

"Naamini mpira ni huru na haki. Kama ni kuotea ni kuotea, na kama sio basi iwe sio, ninaimani hapo baadaye na hata sasa utakuwa wa haki."

Kwenye mchezo huo wa juzi Manchester City iliibuka na ushindi wa jumla ya mabao 4 - 3 dhidi ya Tottenham hata hivyo matokeo hayo hayakuweza kuisaidia timu hiyo kusonga hatua ya nusu fainali kutokana na kufanya matokeo ya jumla kuwa na magoli 4 - 4 Spurs ikinufaika na ushindi wa 0 - 1 nyumbani kwao.

Hata hivyo, City ilifanikiwa kupata bao la tano, lakini lilikataliwa kutokana na mwamuzi kupitia VAR kuona kuwa lilipatikana kwa njia ya kuotea.



# DOND… A SOKA MAGA… A ULAYA




# KLOPP: SIMWAZII MESSI KUELEKEA KUIVAA BARCA

**●●● Afunguka kuhusu ubora wa mshambuliaji huyo ambaye ni raia wa Argentina…**

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp alikuwa na furaha na hakuonyesha hofu yoyote kuhusu kuelekea kukutana na Lionel Messi baada ya kikosi chake kufanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ambapo sasa kitakutana na Barcelona.

**Miamba hiyo ya Ligi Kuu England, Liverpool, juzi Jumatano iliifumua Porto ya Ureno mabao 4-1, katika mechi ya mkondo wa pili ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, hivyo kuitoa kwa jumla ya tofauti ya mabao 6-1.**

Na sasa itakwenda kukutana na Barcelona katika hatua ya nusu fainali, ambayo juhudi za Messi ziliiwezesha kuitoa Manchester United kwa jumla ya mabao 4-0.

Lakini Klopp, alisema Messi, ambaye amefunga mabao 45 msimu huu, amethibitisha haiwezekani kumsimamisha hadi sasa katika michuano hii.

"Hiyo ni vizuri sitakiwi kufikiri kuhusu hilo na nina usiku mchache zaidi," aliuambia mkutano wa wanahabari.

"Kila mmoja amejaribu hilo hadi sasa na hakuna anayeweza kulifanya hilo, lakini tunatazama mbele kwa hilo.

"Kuna kazi nyingi za kufanya kabla ya kukutana na Barcelona. Tutaona."

Wanafainali hao wa msimu uliopita, Liverpool walikuwa wazuri zaidi kuliko Porto katika mechi hiyo ya mkondo wa pili, shukrani kwa mabao kutoka kwa Sadio Mane, Mohamed Salah, Roberto Firmino na Virgil van Dijk.

Klopp ni mwenye msisimko kwa changamoto ya kukutana na Barca, akiongeza kwamba timu yake imetuma "ujumbe mzito" kwa kutinga nusu fainali kwa mara nyingine.

"Tunacheza dhidi ya Barcelona, siwazii sana hukusu hilo, lakini ukweli ni mwenye furaha kuhusu ukweli kwamba tunacheza nao," alisema.

"Tutatafuta vitu ambavyo tunadhani tunaweza kuvitumia, lakini kwa upande mwingine sijali. Tupo nusu fainali, Jumapili tutacheza dhidi ya Cardiff [City], hilo ndilo lililopo akilini mwangu wakati nitakapoamka kesho[jana].

"Tunaweza kutazama timu nyingi ambazo tayari zimejaribu hili, pengine tutapata kitu, lakini ninatazama mbele kwa hili, na si kwa usiku huu tu.

"Ukweli hizo ni taarifa nzuri na ni mwenye furaha kwa watu wote katika klabu. Mwaka wa pili katika nusu fainali ni ujumbe mzito.

"Tunakwenda pale, kila mmoja anajaribu hii. Ukweli ninajisikia fahari kwa vijana hawa. Tumelifanya kwa namna tofauti, hilo linafanya kuwa la kipekee zaidi."

## ZISIKUPITE

### SALAH KUONDOKA LIVERPOOL

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Misri, Mohamed Salah, 26, anataka kuondoka Liverpool na amepanga kuwasilisha ombi la kuachana na klabu hiyo. ***(As.com - Spanish)***

### HAZARD SIKU ZINAHESABIKA

MPANGO wa kiungo wa Chelsea, Eden Hazard, 28, kujiunga na Real Madrid unatarajiwa kukamilishwa siku zijazo na mazungumzo kuhusu nyota huyo wa Ubelgiji kutua Bernabeu yamekuwa yakiendelea kwa miezi minne. ***(Marca)***

### ARSENAL, JUVE KWA NERES

WASAKA vipaji wa Arsenal, wamekuwa wakimtazama mshambuliaji wa Ajax, David Neres, 22, na sasa wanajiunga na Juventus ambayo imeonyesha nia ya kumsajili. ***(Mail)***

### DE LIGT AWINDWA TOTTENHAM

BEKI wa Ajax, Matthijs de Ligt, 19, anawindwa na Tottenham, na ipo tayari kulipa dau kiasi cha pauni milioni 69 zinazohitajika kwa Mholanzi huyo. ***(Star)***

### GIROUD AIGOMEA CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Ufaransa, Olivier Giroud, 32, anajiandaa kukataa ofa ya kuongeza mkataba kwa miezi 12, na sasa anataka kuondoka Stamford Bridge majira ya joto. ***(Mirror)***

### SOLSKJAER KUJAZWA NOTI

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, atapewa pauni milioni 250 za kufanya usajili majira ya joto, ambapo zitatumika kumnunua mshambuliaji wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho, 19. ***(Mirror)***

### POGBA, HAZARD LAO MOJA

KIUNGO wa Ufaransa na Manchester United, Paul Pogba, 26, anajiandaa kujiunga na Eden Hazard katika safari ya kwenda kuitumikia Real Madrid. ***(Sun)***

### RASHFORD, UTD HAKIJAELEWEKA

STRAIKA wa Manchester United, Marcus Rashford, 21, amesita kusaini mkataba mpya hapo Old Trafford, kufuatia nyota huyo wa kimataifa wa England kutaka kulipwa pauni 200,000 kwa wiki. ***(Mail)***

### MALCOM KUGEUZWA CHAMBO

BARCELONA Inataka kumtoa ofa winga Mbrazil Malcom, 22, katika mpango wake wa kumpata Marcus Rashford wa Manchester United. ***(Mundo - in Spanish)***

### HUGHTON 'KIMENUKA' BRIGHTON

MUSTAKABALI wa baadaye wa Kocha wa Brighton, Chris Hughton, upo mashakani klabuni hapo hata kama atafanikiwa kuinusu kushuka daraja. ***(Sun)***

### EVERTON, ARSENAL VITANI

EVERTON na Arsenal zote zinamtaka straika wa Fortuna Dusseldorf na Ubelgiji, Benito Raman, 24, kwa pauni milioni 15. ***(Sport Bild - via Sport Witness)***

### ABRAHAM KURUDI CHELSEA

STRAIKA wa Chelsea, Tammy Abraham, 21, anayecheza kwa mkopo Aston Villa anaweza kurudi Stamford Bridge msimu ujao kuliko kuendelea kuitumikia klabu hiyo. ***(Football.London)***

## Sare zatawala Ligi Kuu Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya JKU imekubali kulazimishwa sare ya mabao 2-2 na "Maafande" wenzao wa Zimamoto katika mchezo wa Ligi Kuu ya Zanzibar uliochezwa juzi jioni kwenye Uwanja wa Amaan Visiwani hapa.

JKU ndio walikuwa wa kwanza kuliona lango la Zimamoto baada ya mchezaji wake, Sheikhu Magasi kufunga bao la kwanza katika dakika ya 24, huku bao la pili likipachikwa na Swedi Juma dakika ya 89 baada ya kupiga mpira wa adhabu.

Mabao ya Zimamoto yenyewe yalifungwa na Haruna Abdallah katika dakika ya 39 na 90, lakini goli la pili la kusawazisha likizua "taharuki" baada ya mashabiki na wachezaji wa JKU kulilalamikia kuwa mpira wote haukuvuka katika mstari wa goli.

Katika mechi nyingine zilizochezwa kwenye Uwanja wa Mau ze dong, Mafunzo na Jang'ombe Boys nao walimaliza dakika 90 kila upande umeshindwa kutingisha nyavu za upande wa pili.

Mbuyuni imefanikiwa kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Hard Rock katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Gombani, Pemba.

Ligi hiyo inatarajia kuendelea tena kesho kwa Jang'ombe Boys kuialika Chuoni kwenye Uwanja wa Mau ze Dong kuanzia saa 10:00 jioni, wakati mapema saa 8: 00 mchana Mafunzo wataikaribisha Zimamoto wakati JKU watavaana na Polisi.

### MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 32 | 23 | 5 | 4 | 51 | 23 | 74 |
| 2. Azam | 31 | 19 | 9 | 3 | 49 | 18 | 66 |
| 3. Simba | 23 | 19 | 3 | 1 | 50 | 8 | 60 |
| 4. Mtibwa Sugar | 32 | 14 | 6 | 12 | 33 | 24 | 48 |
| 5. Lipuli | 33 | 12 | 12 | 9 | 30 | 28 | 48 |
| 6. Kinondoni MC | 31 | 9 | 15 | 7 | 32 | 22 | 42 |
| 7. TZ Prisons | 32 | 10 | 12 | 10 | 26 | 25 | 42 |
| 8. Coastal Union | 33 | 9 | 14 | 10 | 29 | 33 | 41 |
| 9. Mbeya City | 32 | 11 | 7 | 14 | 31 | 34 | 40 |
| 10. Singida United | 33 | 10 | 10 | 13 | 24 | 32 | 40 |
| 11. Ndanda | 31 | 10 | 10 | 11 | 21 | 30 | 40 |
| 12. JKT Tanzania | 32 | 9 | 12 | 11 | 19 | 26 | 39 |
| 13. Stand United | 33 | 11 | 6 | 16 | 30 | 41 | 39 |
| 14. Mwadui | 33 | 10 | 7 | 16 | 37 | 43 | 37 |
| 15. Alliance | 32 | 9 | 10 | 13 | 23 | 33 | 37 |
| 16. Mbao | 33 | 9 | 10 | 14 | 19 | 33 | 37 |
| 17. Kagera Sugar | 32 | 8 | 12 | 12 | 26 | 34 | 36 |
| 18. Ruvu Shooting | 33 | 8 | 12 | 13 | 28 | 39 | 36 |
| 19. Biashara United | 31 | 8 | 10 | 13 | 22 | 29 | 34 |
| 20. African Lyon | 33 | 4 | 10 | 19 | 19 | 43 | 22 |

# SERIKALI YAWAPONGEZA SPORTPESA UJIO WA SEVILLA

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAKATI Kampuni ya Michezo ya Kubashiri ya SportPesa ikiwa tayari imetangaza kukamilika kwa mchakato wa kukileta Tanzania kikosi cha Klabu ya Sevilla ya Hispania kwa ajili ya ziara ya kimichezo itakayohusisha kucheza mechi moja dhidi ya Simba au Yanga, mpango huo umepokelewa kwa mikono miwili na pongezi juu kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, imeelezwa.

Mkurugenzi wa Utawala na Utekelezaji wa Kampuni ya SportPesa, Abbas Tarimba, juzi jijini Dodoma alitangaza kuwa kampuni hiyo kwa kushirikiana waendeshaji wa Ligi Kuu Hispania, La Liga, wamefanikisha mchakato wa Sevilla kufanya ziara ya kimichezo nchini ikiwa ni sehemu ya maandalizi yake ya msimu mpya na kwamba kikosi hicho chenye historia ya kutwaa ubingwa wa Uefa Europa League mara tano, kitawasili nchini Mei 21, mwaka huu na kucheza mechi moja kati ya Simba ama Yanga siku mbili baadaye.

Hata hivyo, wakati wa kutangazwa kwa ujio huo kuligeuka gumzo kwa wadau wa soka nchini, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Khamis Kigwangalla, amesema ujio wa Klabu ya Sevilla ni fursa kubwa ya kuitangaza nchi kupitia vivutio vya maliasili.

**Akizungumza jijini Dodoma baada ya SportPesa kutangaza kuileta Sevilla, alisema ujio huo unatosha kabisa kwa dunia kuijua Tanzania kutokana na ukubwa wa klabu hiyo yenye mashabiki wengi.**

Kigwangalla alisema, kwa sasa watu wengi duniani watataka kuijua Tanzania na kuonekana kila kona duniani, hivyo ni fursa kwa nchi kutangaza utalii uliojaliwa kupitia wachezaji hao.

Alisema serikali imepanga kuitumia fursa hiyo kwa kushirikiana na SportPesa kwa lengo la kutangaza vivutio vya nchi kabla na baada ya mechi hiyo kuchezwa dhidi ya Simba ama Yanga.

"Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Utalii na Maliasili, hii ni fursa yetu tunayotakiwa kuitumia vema kuitangaza nchi kupitia ziara ya Sevilla kuwaleta nchini mabingwa hao mara tano wa michuano ya Uefa Europa League ikiwa ni sehemu ya maandalizi yao ya msimu mpya wa 2019/2020.

"Kwa kupitia Sevilla yenye wachezaji wakubwa wa kimataifa, kutasaidia kuitangaza nchi watakapokwenda kutembelea vivutio vyetu vya asili tulivyojaliwa hapa nchini zikiwamo mbuga mbalimbali.

"Wachezaji hao watakapokuwa kwenye hifadhi zetu misitu ya mbugani watapiga picha ambazo watazisambaza kwenye mitandao, ambapo mashabiki watataka kuhoji ni wapi walipo na kwa nini wapo kwenye pori lenye wanyamapori, na baadaye na wao kuvutiwa na kuja nchini.

"Kwa kufanya hivyo, tutaongeza idadi ya watalii kuja nchini kutembelea na ninajua watataka kwenda Zanzibar kutembelea huko, pia ni fursa nzuri ya kutangaza utalii huko.

"Kwa kupitia ziara hiyo, tumetoa ofa kwa Sevilla kwa kuwapeleka kwenye moja ya hifadhi zetu bure watakapofika hapa nchini," alihitimisha Kigwangalla.




Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Benki ya NMB, Juma Kimori (kushoto), akimkabidhi msaada wa fulana 250 Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Magereza (SACP) Bertha Mende, kwa ajili ya wanamichezo wa Jeshi la Magereza Tanzania watakaoshiriki katika Tamasha la Pasaka litakalofanyika Unguja, Zanzibar kuanzia leo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Malindi yaendelea kujipa matumaini*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA wa Malindi, Salehe Machupa, amesema kuwa bado anaimani na timu yake kuwa inaweza kufanya vizuri katika michezo yake iliyobakia ya Ligi Kuu Zanzibar licha ya kukabiliwa na wachezaji saba majeruhi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Machupa, alisema timu yake ina kikosi kipana ambacho kinaweza kupata matokeo mazuri na hata kufanikiwa kunyakuwa ubingwa wa ligi hiyo katika msimu huu.

Machupa alisema kuwapo kwa majeruhi hao saba hakuwezi kupunguza kasi ya kikosi chake katika mechi zinazofuata za ligi hiyo kwa sababu ana wachezaji wenye uwezo na watakaoziba pengo la wenzao walioumia.

"Tutawakosa wachezaji saba kutokana na kuwa majeruhi, lakini hii haimaanishi upungufu huo utatufanya tufungwe, hapana lengo letu bado lipo pale pale la kuhakikisha tunashinda michezo yote iliyobakia ili tujiweke katika nafasi nzuri zaidi na ikiwezekana kunyakuwa ubingwa," alisema Machupa.

Aliwataja baadhi ya wachezaji wake ambao ni majeruhi ni pamoja na John Otieno, Ali Mabata, Abuobakar Guti na Mohammed Krick.

Hata hivyo amewataka mashabiki wa timu hiyo kuendelea kuwapa ushirikiano katika kuiendesha klabu hiyo na hasa kufika uwanjani kuwashangilia ili waweze kutimiza malengo yao.

# Michezo

Ijumaa Aprili 19, 2019

Nipashe




Klopp: Simwazii Messi UKURASA 30



Mshambuliaji wa Tottenham, Dele Alli (kulia), akifanikiwa kumtoka beki wa Manchester City, David Silva, katika mechi ya marudiano ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa juzi usiku. City ilishinda mabao 4-3 lakini ilitolewa katika michuano hiyo kutokana na kufungwa goli 1-0 katika mchezo wa kwanza. **PICHA: MTANDAO**

## Mengi apongezwa mafanikio ya Serengeti Boys

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, amempongeza Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, kwa msaada mkubwa alioutoa kwa Timu ya Taifa ya Vijana (Serengeti Boys) na kwa wizara hiyo.

Akiwasilisha hotuba bungeni jijini hapa jana, kuhusu makadirio ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Dk. Mwakyembe alisema Dk. Mengi ni mlezi wa timu hiyo na ameilea kwa hali na mali.

Alisema ushiriki wa timu hiyo kwenye Kombe la Cosafa kwa kiasi kikubwa uliwezeshwa na Dk. Mengi.

"Natoa shukrani maalum kwa wafanyabiashara wawili, Mzee Reginald Mengi, Mwenyekiti Mtendaji wa IPP na Mzee Subhash Patel, Mwenyekiti wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania - CTI) kwa msaada mkubwa walioutoa kwa Serengeti Boys na kwa wizara," Dk. Mwakyembe alisifu.

Alibainisha kuwa Subhash ameipatia wizara yake katoni 11,000 za maji na juisi, ametoa kwa maofisa wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF) vyumba vya kulala 27 na vingine vya kufanyia kazi katika hoteli ya nyota tano kwa kipindi chote cha mashindano ya Afrika (Afcon U-17) yanayoendelea jijini Dar es Salaam.

"Subhash pia ametuturuhusu tuweke timu za nchi tatu hoteli ya Whitesands kwa siku 14 bila malipo. Nikishindwa kutambua mchango huo adhimu katika hotuba yangu, basi nitakuwa nanyemelewa na roho ya kichawi," alisema.

Waziri huyo pia alizishukuru kampuni za Sahara Energy na Engen kwa msaada wa mafuta ya magari yote yanayotumika katika mashindano ya Afcon -U17.

Wakati huo huo, Timu ya Vijana ya Cameroon imepata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Morocco katika mechi ya Kundi B iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jana na kujiweka katika mazingira mazuri ya kusonga mbele katika michuano hiyo.

# Aussems: Kiu yetu ubingwa

**Na Somoe Ng'itu**

## Tutapambana hadi mechi ya mwisho, kutua Bukoba kwa mafungu...

BAADA ya timu yake kupata ushindi wa mechi ya 11 mfululizo za Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Simba ya jijini Dar es Salaam, Patrick Aussems, amesema kuwa kiu ya kikosi chake ni kutetea ubingwa wa ligi hiyo ambayo sasa iko katika hatua za lala salama.

**Akizungumza na Nipashe jijini Tanga, Aussems, alisema kuwa timu yake imebakia katika shindano moja tu msimu huu, nalo ni Ligi Kuu, hivyo hawatakubali kuona wanaipoteza nafasi ya kushinda taji hilo kwa mara ya pili mfululizo.**

Aussems alisema kuwa wachezaji wake wataendelea kupambana katika kila mechi watakayocheza ili waweze kukusanya pointi zaidi, licha ya kukabiliwa na ratiba ngumu kwenye ligi hiyo ambayo inatoa tiketi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika kwa upande wa Tanzania Bara.

Mbelgiji huyo alikiri kuwa hakuna mechi rahisi ambayo watacheza, kwa sababu kila timu watakayokutana nayo ina malengo yake na hali hiyo huongeza ushindani.

"Malengo na ndoto na kiu yetu ni kuwa mabingwa wa ligi, tulitolewa katika Kombe la FA na wiki iliyopita pia tuliiaga michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tunahitaji tena kushiriki mashindano hayo ya kimataifa mwakani na njia yake ni kutwaa ubingwa, tutapambana ili kupata nafasi hii," alisema kocha huyo.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, alisema kuwa Simba ilistahili kupata ushindi katika mchezo dhidi yao kutokana na kiwango kizuri walichokionyesha katika mchezo huo.

Mgunda alisema kuwa wachezaji wa Simba wameimarika zaidi kutokana na uzoefu walioupata kutoka kwenye mechi za kimataifa na kutumia makosa ya nyota wake kupata ushindi. Naye meneja wa timu hiyo, Patrick Rweyemamu, aliliambia gazeti hili kuwa kikosi cha kwanza cha timu hiyo chenye wachezaji 18 kitaondoka leo kuelekea Bukoba kwa ajili ya kuwafuata wenyeji wao, Kagera Sugar na nyota wengine waliosalia wataondoka kesho.

"Tutaondoka Dar es Salaam kesho (leo), ila wachezaji wengine wanne wao watakuja Jumamosi (kesho), katika orodha hiyo tutamkosa Wawa (Paschal) ambaye bado hajapona vema," alisema meneja huyo.

Simba yenye pointi 60 baada ya kucheza michezo 23 itakutana na wenyeji wao Kagera Sugar ambao wana pointi 36 wakishuka uwanjani mara 32.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002